



BILA KUPINGWA, BILA KUKOSOLEWA, BILA HAKI

“WIMBI LA HOFU” LAIKUMBA TANZANIA KUELEKEA UCHAGUZI 2025

TAARIFA YA
UTAFITI

AMNESTY
INTERNATIONAL



YALIYOMO

FAHARASA	3
1. MUHTASARI	4
2. MBINU	5
4.1 SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA ZA VYAMA VYA SIASA, 2024	7
4.2 SHERIA YA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI, 2024	7
4.3 MAREKEBISHO YA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI MTANDAONI), 2025	8
5. HAKI YA KUIISHI NA USALAMA WA MTU	8
6. UTESWAJI NA UKATILI MWINGINE	9
7. UTEKWAJI NA UTOWESHWAJI	11
8. UWEKWAJI KIZUIZINI BILA KUFUATA TARATIBU ZA KISHERIA NA MASHTAKA YASIYOZINGATIA SHERIA	14
9. UKIUKWAJI WA HAKI YA KUKUSANYIKA KWA AMANI	16
10. USHAMBULIWAJI WA UHURU WA KUJIELEZA NA VYOMBO VYA HABARI	19
11. UMINYWAJI WA UHURU WA KUTEMBEA	22
11.1 kudharau uhuru wa kutembea uliopo kimkataba	23
12. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	23
12.1 kwa rais wa jamhuri ya muungano wa TANZANIA	24
12.2 kwa waziri wa mambo ya ndani	25
12.3 kwa waziri wa habari, utamaduni, sanaa na michezo	25
12.4 kwa waziri wa katiba na sheria	25
12.5 kwa tume huru ya taifa ya uchaguzi	26
12.6 kwa vyama vyote vya siasa na wagombea wote	26
12.7 kwa waangalizi wa uchaguzi	26
12.8 kwa jumuiya ya afrika mashariki	27
12.9 kwa jumuiya ya maendeleo kusini mwa afrika	27
12.10 kwa umoja wa afrika	27
12.11 kwa jumuiya ya kimataifa	28

Askari wa kupambana na ghasia wa Zanzibar wakiwa wamewaweka chini ya ulinzi watu kadhaa baada ya upinzani kufanya maandamano Stone Town, mnamo Oktoba 29, 2020, kutokana na mvutano ulioibuka wakati wa kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi mkuu. ©MARCO LONGARI/AFP via Getty Images).

Licha ya tahadhari za hapo awali kupitia ripoti ya Amnesty International ya mwaka 2020, mamlaka za Tanzania zimeongeza ukandamizaji, zikitumia sheria tata na zenye madaraka makubwa kunyamazisha upinzani kuelekea uchaguzi wa Oktoba 2025. Kati ya Januari 2024 na Oktoba 2025, Amnesty imeonesha unyanyasaji mkubwa, ikiwemo utoweshwaji, ukamatwaji bila kufuata utaratibu wa kisheria, uteswaji na ukatili mwingine na mauaji bila amri ya mahakama. Uhuru wa kujieleza, kutembea, na kukusanyika kwa

FAHARASA

NENO	MAELEZO
ACT-WAZALENDO	Chama cha upinzani Tanzania; Alliance for Change and Transparency – Wazalendo
ACHPR	Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu
AU	Umoja wa Afrika
AUEOM	Ujumbe wa Waangalizi wa Uchaguzi wa Umoja wa Afrika
CCM	<i>Chama Cha Mapinduzi</i> – chama tawala Tanzania
CHRAGG	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora – taasisi ya haki za binadamu Tanzania
CSO	Asasi ya Kiraia
DCI	Mkurugenzi wa Uchunguzi wa Mashtaka ya Jinai – chombo cha sheria Tanzania
EAC	Jumuiya ya Afrika Mashariki
EACJ	Mahakama ya Afrika Mashariki
ED	Kutoweshwa
ICCPR	Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kiasiasa
ICRC	Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu
INEC	Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi – chombo cha uchaguzi Tanzania, zamani NEC.
IHL	Sheria ya Kimataifa ya Masuala ya Kibinadamu
JAMIIFORUMS	Jukwaa la mtandaoni nchini linalofahamika kwa kutoa taarifa na mijadala ya umma
MP	Mbunge
NEC	Tume ya Taifa ya Uchaguzi – jina la zamani la chombo cha uchaguzi, sasa INEC
NGO	Shirika Lisilo la Kiserikali
OHCHR	Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu
RIG	Mwongozo wa Kisiwa cha Robben – mwongozo wa Umoja wa Afrika kuhusu kukataza na kuzuia utesaji
SADC	Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika
TLS	Chama cha Wanasheria wa Tanganyika – chama cha mawakili wa Tanzania bara
TCRA	Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania
UDHR	Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu
UNCAT	Mkataba wa Umoja wa Mataifa Dhidi ya Utesaji
WGEID	Kikosi Kazi cha Umoja wa Mataifa kuhusu Kutoweshwa au Kupotezwa Bila Hiari
X	Zamani Twitter

1. MUHTASARI

Tanzania inaendelea kushuhudia ongezeko kubwa la tatizo la haki za binadamu kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba 2025. Licha ya gunduzi na mapendekezo yaliyotolewa na Amnesty International katika ripoti yake ya mwaka 2020 *“Matumizi ya Sheria Kama Silaha: Ukandamizaji wa Kisheria Kabla ya Uchaguzi Mkuu Tanzania”* iliyoangazia hali ya kutia wasiwasi kuhusu haki za binadamu kuelekea uchaguzi na kutoa wito kwa mamlaka za Tanzania kuheshimu na kuzingatia haki za binadamu katika kipindi chote cha kupiga kura na baada ya hapo¹, hali imekuwa mbaya zaidi wakati nchi ikielekea katika uchaguzi wa mwaka huu. Mamlaka zimezidisha kwa kiwango kikubwa matumizi ya sheria kandamizi kunyamazisha upinzani, zikilenga maandishi wa habari, asasi za kiraia, watetezi wa haki za binadamu, na sauti za upinzani.

Kati ya Januari 2024 na Oktoba 2025, Amnesty International imeorodhesha ukiukaji mkubwa na wa kimkakati wa haki za binadamu, ikiwemo utoweshwaji, utiwaji mbaroni bila kufuata taratibu za kisheria, utesaji, mauaji kinyume cha sheria, na uminywaji mkubwa wa uhuru wa kutembea, kujieleza, na kukusanyika. Matendo haya yanaonesha mkakati wa makusudi wa kuzuia ushiriki wa raia na kushikilia madaraka, ukidhoofisha haki ya msingi ya Watanzania na kudhoofisha ubora wa mchakato wa kupiga kura.

Taarifa hii inaangazia jinsi mfumo wa sheria wa Tanzania usivyokuwa na kinga ya kuwalinda wanasiasa na raia dhidi ya kuonewa na dola. Sheria zisizokuwa na tafsiri bayana na zenye matumizi mapana zinawezesha matumizi ya kibaguzi, zikidhoofisha ushiriki wa kidemokrasia na ukiukwaji wa viwango vya kimataifa vya haki za binadamu. Taarifa hii inatokana na maelezo yaliyothibitishwa kutoka vyanzo mbalimbali, wakiwemo wahanga, mashahidi, familia, wawakilishi wa kisheria, makundi ya asasi za kiraia, na vyombo vya habari. Mbinu ya kawaida ya Amnesty International ilitumika, ikitoa kipaumbele kwa uhakika wa chanzo, usalama na usiri. Majina ya wachangiaji wengi yalifichwa kutokana na hofu ya kulipiziwa kisasi.

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) iliidhinisha wagombea urais 17, akiwemo Rais Samia Suluhu Hassan. Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), chama kikuu cha upinzani, kilienguliwa kutoshiriki uchaguzi kwa kukataa kusaini Kanuni za Maadili ya Uchaguzi. Mgomba urais wa ACT Wazalendo, Luhaga Mpina, ambaye alihama kutoka chama tawala CCM, aliteuliwa na ACT Wazalendo kama mgomba wao wa urais naye pia alienguliwa na INEC licha ya kushinda kesi mahakamani, na kufanya chama tawala cha CCM kuwa na upinzani mdogo katika uchaguzi wa mwaka 2025, kwa kuwa washindani wakubwa wawili wameenguliwa. Msajili wa Vyama vya Siasa alibatilisha ugombea wa Mpina, akitaja ukiukwaji wa taratibu za ndani za chama, na kusema kwamba Mpina hakuna mwanachama wa ACT Wazalendo kwa kipindi hitajika kisichopungua siku 30 na aliteuliwa baada ya tarehe ya mwisho ya chama.² Chama hicho kilidai kanuni zake zilikuwa zimeboreshwa.

Sheria kadhaa, ikiwemo Sheria ya Marekebishio ya Sheria za Vyama vya Siasa, 2024, Sheria ya Makosa ya Mtandao, na Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, zimekuwa zikitumika kufanya ukosoaji kuwa kosa la jinai, kusimamia maudhui ya vyombo vya habari, na kudhibiti uhuru wa kidigitali. Usimamiaji wa maudhui ya vyombo vya habari na mitandao uliendelea kuwa mkubwa sana wakati wa kipindi hiki wakati maandishi wa habari na watengeneza maudhui mtandaoni wakiendelea kukamatwa, kufungwa, na kufuatiliwa. Mtinge maudhui mwenye miaka 24 alipotea wakati mwingine akitoa taarifa ya kutekwa na kuteswa. Majukwaa maarufu ya mitandao ya kijamii ambayo Watanzania wanayategemea kwa kupata habari kama vile JamiiForums na X nayo pia yalizuiwa na yataendelewa kuzuiwa wakati wa kipindi cha uchaguzi.

Utoweshwaji na mauaji pia yametumika na serikali kunyamazisha wakosoaji wake huku matukio kadhaa ya utekaji na mauaji bila amri ya mahakama ya viongozi wa upinzani na wanaharakati yakiripotiwa, huku kukiwa na uwajibikaji mdogo na hata kutokuwajibika kabisa. Wanaharakati na

¹ Amnesty International, *“Tanzania: Kutumia Sheria kama Silaha: Ukandamizaji wa Sheria kuelekea Uchaguzi Mkuu Tanzania,”* Oktoba 20, 2020, www.amnesty.org/en/documents/afr56/3051/2020/en/

² Kanuni za Ndani za ACT-Wazalendo 2015.

wanachama wa vyama vya upinzani pia wamekuwa wakiteswa, wakiwekwa kizuini bila ya kuwasiliana na waliopo nje, na mashtaka yanayochochewa na siasa, ikiwemo uhaini.

Uhuru wa kutembea na kukusanyika kwa amani umekandamizwa kutokana na mamlaka kutumia madaraka yasiyotokana na utaratibu wa kisheria kuzuia viongozi wa upinzani kusafiri, kupiga marufuku mikutano ya kisiasa, na kutawanya kwa nguvu watu waliokusanyika kwa amani ikiwemo katika nyumba za ibada.

2. MBINU

Taarifa hii inatokana na ukusanyaji mkubwa wa taarifa kimaandishi kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu uliotokea nchini Tanzania kati ya Januari 2024 na Oktoba 2025. Mbinu za utafiti zinazingatia utaraibu wa kawaida wa Amnesty International wa kuorodhesha haki za binadamu, kwa msisitizo wa kulinda usalama na usiri wa vyanzo. Taarifa hii imekusanywa kutokana na vyanzo mbalimbali, ikiwemo ushahidi wa wahanga, maelezo ya mashuhuda, wanafamilia, wawakilishi wa kisheria, asasi za kiraia, na taarifa za vyombo vya habari. Matukio yote yaliyoorodheshwa yamethibitishwa kupitia vyanzo mbalimbali vya kujitegemea pale ilipowezekana.

Amnesty International pia ilifanya utafiti mkubwa wa kiofisini ikipitia picha mjongeo, picha mnato, taarifa rasmi na taarifa za vyombo vya habari. Ushahidi zaidi ulipatikana kutoka vyanzo vingine rasmi, ikiwemo tovuti za serikali, ambazo zilitoa muktadha wa ziada na uthibitishwaji wa gunduzi.

Mnamo Oktoba 6, 2025, Amnesty International ilituma barua kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiomba majibu rasmi kwa maswala mahsusi ambayo tumeyafanyia uchunguzi. Hadi wakati wa kuandaa taarifa hii, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikuwa bado hajatumia haki ya kujibu.

Kwa jumla, watu 43 walihojiwa wakati wa kufanya utafiti huu. Wahojiwa wote walitoa ridhaa ya kutumia maelezo yao. Pale wahojiwa walipokuwa na wasiwasi kuhusu hofu ya kulipiziwa kisasi, majina yao na taarifa nyingine ambazo zingeweza kuwatambulisha ziliachwa ili kulinda utambulisho na usalama wao.

3. USULI

Kufuatia kifo cha Rais John Magufuli Machi 2021, Samia Suluhu Hassan alikuwa rais wa kwanza mwanamke Tanzania. Licha ya kuwepo na matumaini ya awali ya mabadiliko, serikali imeendeleza na kuongeza zaidi matukio ya ukandamizaji yanayolenga viongozi wa upinzani, asasi za kiraia, waandishi wa habari, na sauti nyingine zenye mawazo tofauti.

Mnamo Juni 13, 2025, wataalamu wa Umoja wa Mataifa wa haki za binadamu waliitaka Tanzania kukomesha mara moja utoweshwaji wa wapinzani wa kisiasa, watetezi wa haki za binadamu na waandishi wa habari, kama njia ya ukandamizaji katika muktadha wa uchaguzi. Wataalamu wa Umoja wa Mataifa waliorodhesha ukiukwaji mwingine wa haki za binadamu unaotumika kama njia ya ukandamizaji kuwa ni pamoja na, “kutiwa mbaroni bila kufuata utaratibu wa sheria, unyanyasaji, utesaji na utoweshwaji wa viongozi vijana, watetezi wa haki za binadamu, na wanachama wa vyama vya siasa vya upinzani.”³

Wakati Tanzania ikijiandaa kwa uchaguzi mkuu mnamo Oktoba 29, 2025, chama tawala, *Chama Cha Mapinduzi* (CCM), ambacho ni cha pili Afrika kwa kuwa madarakani kwa muda mrefu zaidi, kinakabiliwa na upinzani kidogo wakati wa uchaguzi. Chini ya Rais Hassan, mamlaka zimeongeza kasi ya kampeni inayoratibiwa ya kukandamiza upinzani wa kisiasa na mawazo tofauti. Tundu Lissu, Mwenyekiti wa Chadema, yupo rumande akikabiliwa na shataka la uhaini kutokana na kauli aliyoitoa Aprili 3, 2025, akiwataka wafuasi wake kugomea uchaguzi. Kushtakiwa kwake kunaonesha ukandamizaji mkubwa dhidi ya mawazo mbadala na kupungua kwa nafasi ya kushiriki katika masuala ya siasa.

Mnamo Aprili 12, 2025, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) ilikiondoa Chadema kushiriki kwenye uchaguzi baada ya chama hicho kukataa kusaini Kanuni za Maadili ya Uchaguzi ambalo ni jambo la lazima ikitoa sababu ya wasiwasi ambao haujasuluhishwa kuhusu uadilifu wa uchaguzi. Kuenguliwa huko kunahusu chaguzi zote hadi mwaka 2030.

Katika kudhoofisha zaidi siasa ya vyama vingi, Msajili wa Vyama vya Siasa alifuta uhalali wa uteuzi wa sekreteriati ya Chadema mnamo Mei 13, 2025, akiwavua viongozi muhimu nafasi zao. Ingawa Mahakama Kuu ilitengua uamuzi huo mnamo Agosti 28, Msajili amekataa kutekeleza amri.

Mgombea urais wa ACT-Wazalendo, Luhaga Mpina, pia alienguliwa na INEC mnamo Agosti 7, akitaja kutozingatia kanuni. Kuenguliwa kwake kulifuatia kuhama kutoka chama tawala cha CCM. Mahakama Kuu ilitoa uamuzi kuwa kuenguliwa huko kulikuwa kinyume cha Katiba mnamo Septemba 11, ikisisitiza Mpina kupewa haki ya kusikilizwa. Hata hivyo, INEC ilimuengua tena mnamo Septemba 15 kufuatia pingamizi la Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kuenguliwa kwa Lissu na Mpina kunaangazia ongezeko la wasiwasi kuhusu uhuru wa taasisi za uchaguzi kuelekea zoezi la kupiga kura sasa ambapo washindani wakuu wa kisiasa hawamo.⁴

Mfumo wa sheria wa Tanzania unaendelea kuwezesha ukandamizaji. Mamlaka zimetumia sheria kama silaha, ikiwemo Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sheria ya Vyama vya Siasa, Sheria ya Makosa ya Mtandaoni, na Sheria ya Utulivu wa Umma, kunyamazisha mawazo tofauti, kuminya uhuru, na kukomaza utawala wa kimabavu. Sheria hizi hazina tafsiri bayana, zina wigo mpana sana, na haziendani na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.

³ Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu (OHCHR), Tanzania: Wataalamu wa UN washtushwa na mtindo wa utoweshwaji na utesaji ili kunyamazisha upinzani na wakosoaji, Juni 13, 2025, www.ohchr.org/en/press-releases/2025/06/tanzania-un-experts-alarmed-pattern-enforced-disappearance-and-torture

⁴ Taasisi ya Kimataifa ya Demokrasia na Usaidizi wa Uchaguzi (International IDEA), Tanzania - Agosti 2025: Mgombea urais wa upinzani azuliwa kabla ya uchaguzi wa Oktoba, Agosti 2025, www.idea.int/democracytracker/report/tanzania/august-2025

4. MUKTADHA WA KISHERIA

Kuelekea kipindi cha uchaguzi, mamlaka za Tanzania zimetunga sheria na kanuni, ambazo, ingawa ziliwasilishwa kama zenye lengo la kuleta mabadiliko ya kiutawala au maadili, kwa pamoja zinatumiwa kuminywa upinzani wa kisiasa, kukandamiza mawazo tofauti, na kuongeza udhibiti wa serikali kuhusu haki ya uhuru wa kujieleza, kujumuika na kukusanyika kwa amani. Sheria hizo, kuanzia mabadiliko ya uchaguzi hadi sheria za kuchunguza maudhui mtandaoni, zinaweka vikwazo vya kiurasimu, mifumo ya ufuatiliaji, na mamlaka ya utekelezaji kwa hiari ambayo yanaathiri zaidi vyama vya upinzani, asasi za kiraia (CSO), na vyombo huru vya habari. Kuenguliwa kwa Chadema kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kwa kukataa kusaini Kanuni za Maadili ya Uchaguzi ni mfano wa jinsi sheria hizi zinavyotumika kuondoa sauti zenye mawazo tofauti kutoka kwenye mchakato wa kidemokrasia. Hapo chini ni baadhi ya hizo sheria kwa ufupi:

4.1 SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA ZA VYAMA VYA SIASA, 2024⁵

Sheria hii, ambayo ilisainiwa na rais mnamo Machi 7, 2024, na kuanza kutumika Machi 22, 2024, imeanzisha matakwa mengi mapya ya kiurasimu kwa vyama vya siasa, na kutengeneza mianya mingi kwa serikali kuingilia shughuli za vyama vya siasa. Sheria hii, inayofahamika kama Sheria Na. 3 ya mwaka 2024, inavitaka vyama vya saisa kwa lazima kuwa na kanuni thabiti kimaandishi, ikiwemo sera za ujumuishwaji kijinsia na kijamii, kanuni za usimaamizi wa fedha, kanuni za ununuzi, na kanuni za ajira. Wakati kanuni hizi zinaweza kuonekana ni za kiutawala, zinatoa mwanya wa usimamizi wake kiubaguzi dhidi ya vyama vya upinzani na kuweka mzigo mkubwa wa utekelezaji ambao unaweza kutumika kuhalalisha chama kufutwa au kupewa adhabu. Chadema kilizuiwa kufanya shughuli za kisiasa kufuatia ombi la zuio mahakamani. Sheria hii iliyofanyiwa marekebisho inatoa madaraka makubwa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, ikimuwezesha kuweka mazuio kama hayo kwa msingi wa madai ya kuwepo tofauti za ndani au ukiukwaji. Sheria hii ilitajwa katika kesi iliyofunguliwa mahakamani na wadhamini wa Chadema kutoka Zanzibar, wakidai kutokuwepo na mlingano katika ugawaji wa rasilimali na ukiukwaji wa kanuni za uongozi wa chama. Kesi hiyo ilisababisha Mahakama Kuu kuiweka Chadema zuio la kuendesha shughuli zake.⁶

4.2 SHERIA YA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI, 2024⁷

Sheria hii ilisainiwa na Rais mnamo Machi 22, 2024, na kuanza kutumika Julai 10, 2024, ikibadili jina la Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), hususani kwa ajili ya kuimarisha kujitegemea kwake. Hata hivyo, sheria hii inaweka uteuzi wa nafasi zake muhimu chini ya Rais, ikimruhusu kuteua moja kwa moja wajumbe watano kati ya wajumbe kumi wa tume. Kipengele hiki kimepingwa hususani na upinzani kwa vile kinadhoofisha uhuru wa kweli kuelekea uchaguzi wa mwaka 2025, na ndiyo msingi wa kampeni ya Chadema ya “Bila Mabadiliko, Hakuna Uchaguzi.”

Mnamo Agosti 26, 2025, Msajili wa Vyama vya Siasa, mteule wa rais, alibatilisha uteuzi wa Luhaga Mpina kama mgombea urais wa *ACT-Wazalendo*. Uamuzi huu ulitokana na madai ya ukiukwaji wa utaratibu wa ndani ya chama, akisema kwamba Mpina hakuwa mwanachama kipindi kinachotakiwa kisichopungua siku 30 na aliteuliwa baada ya tarehe ya mwisho rasmi ya chama.⁸ *ACT-Wazalendo* ilipinga uamuzi huu, ikidai kwamba kanuni zake za ndani zilikuwa zimeboreshwa, na kufanikiwa kupinga kuengeuliwa katika Mahakama Kuu ya Dodoma. Mnamo Septemba 11, mahakama iliamua kwamba kuenguliwa kwa Mpina kulikuwa kinyume na Katiba na kuamuru INEC kumrejesha kama

⁵ Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa, 2024*, Sheria Na. 3 ya 2024, imetungwa Machi 7, 2024, imeanza kutumika Machi 22, 2024. Inapatikana kupitia: <https://tanzlii.org/akn/tz/act/2024/3>

⁶ The Citizen, Wadhamini wa Chadema kutoka Zanzibar waishitaki Chadema wakidai kutokuwepo mlingano katika kugawa rasilimali, Aprili 17, 2025, www.thecitizen.co.tz/tanzania/news/court-news/zanzibar-trustees-sue-chadema-over-alleged-discrimination-resource-misallocation-5006136

⁷ Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, 2024*, imeanza kutumika Julai 10, 2024. Inapatikana kupitia: oagmis.oag.go.tz/storage/index-attachments/parliamentary-acts/pwRfK7NjyHYUrql1EYia2LEPG73imjVv1yKYhj8.pdf

⁸ Kanuni za Ndani za ACT-Wazalendo 2015.

mgombea na kuanza tena mchakato wa uteuzi. Hata hivyo, mnamo Septemba 15, INEC ilikataa kutii, ikitoa sababu mpya za kisheria ambazo zilitolewa na Mwanasheria Mkuu, ambazo kwa mujibu wa tume zilihalalisha Mpina kuenguliwa.⁹

4.3 MAREKEBISHO YA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI MTANDAONI), 2025

Marekebisho ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni), 2025 ambayo yalifanyia mabadiliko Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni), 2020 yalipitishwa kuwa sheria mnamo Januari 28, 2025. Marekebisho hayo yanawakilisha mwendelezo wa juhudi za serikali kudhibiti mawasiliano ya kidigitali na maudhui ya mtandaoni.¹⁰ Marekebisho hayo yanaweka matakwa makali ya uzingatiji zaidi kwa watoa maudhui ya mtandaoni na kupanua mifumo ya udhibiti, na kuweka vikwazo vya ziada vya kujieleza kwa uhuru na kubadliishana habari. Kanuni hizo zinafanya kazi kwa ushirikiano na sheria zilizopo kuunda mfumo thabiti wa kuchuja maudhui ya kidigitali. Mabadiliko hayo yanawataka watengeneza maudhui ya mtandaoni kuweka mifumo ya kutambua vyanzo vya habari, kimsingi kuondoa kabisa usiri kwa mawasiliano ya kidigitali na kutengeneza mifumo ya doria mtandaoni na kuwachukulia hatua wakosoaji.

Mnamo Mei 27, 2025, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), chombo cha serikali kinachosimamia mawasiliano ya simu, utangazaji, intaneti, na huduma za posta nchini Tanzania ilitoa agizo kwa The Chanzo Initiative, jukwaa huru la habari kuondoa video ya mkutano na waandishi wa habari uliofanywa na Josephat Gwajima, Mbunge wa CCM anayejulikana kwa kupinga uongozi wa chama na sera za serikali. Video hiyo, iliyochapishwa kwenye chaneli ya YouTube ya The Chanzo Initiative, ilimuonesha Gwajima akizungumza kuhusu madai ya utekwaji na utoweshwaji nchini Tanzania.¹¹

5. HAKI YA KUISHI NA USALAMA WA MTU

“Kila mwanadamu ana haki yakaheshimiwa maisha yake na utu wake.”¹²

Mnamo Septemba 6, 2024, Ali Mohammed Kibao, mwanamikakati mwandamizi wa Chadema mwenye miaka 69, alitekwa kutoka katika basi jijini Dar es Salaam wakati wa mchana na kuendelea kutoonekana kwa saa kadhaa kabla ya mwili wake kukutwa umetupwa karibu na pwani ya Bahari ya Hindi asubuhi iliyofuatia. Kibao alikuwa ameuawa kikatili, uso wake ukiwa umeharibika kwa kumwagiwa tindikali, ikionesha dhahiri alikuwa ameteswa.¹³ Ingawa Rais Hassan aliagiza¹⁴ uchunguzi ufanyike haraka kuhusu mauaji ya Kibao¹⁵, hakuna maendeleo yanayoonekana kwamba uchunguzi unafanyika. Mnamo Oktoba 25, 2024, familia ya Kibao ililalamika kwamba polisi wa Tanzania hawakuwa wameonesha dhamira ya kufanya uchunguzi wa kesi hiyo,

⁹ Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Uamuzi dhidi ya Pingamizi la Uteuzi wa Wagombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Septemba 15, 2025, www.inec.go.tz/news/uamuzi-wa-pingamizi-za-uteuzi-wa-wagombea-wa-kiti-cha-rai-kwa-jamhuri-ya-muungano-wa-tanzania

¹⁰ Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *Marekebisho ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni), 2025*, Tangazo la Serikali Na. 57 la 2025, Januari 28, 2025. Yanapatikana kupitia: <https://www.tcra.go.tz/uploads/documents/sw-1738833320-Online%20Content%20Amendment%20Regulations,%202025%20GN%20No%2057%20of%2028%20January%202025.pdf>

¹¹ The Chanzo, *The Chanzo Yaondoa Maudhui ya Askofu Gwajima Kufuatia Wito wa TCRA*, Mei 27, 2025, thechanzo.com/2025/05/27/the-chanzo-yaondoa-maudhui-ya-askofu-gwajima-kufuatia-wito-wa-tcra

¹² Ibara ya 4 ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (Mkataba wa Afrika).

¹³ The Chanzo, “Kada wa Upinzani Aliyetekwa Akutwa Amekufa, Rais Aagiza Uchunguzi Ufanyike. Makada Watatu Waliotekwa Hivi Karibuni Bado Hawajulikani Walipo,” Septemba 8, 2024, thechanzo.com/2024/09/08/abducted-tanzanian-opposition-leader-found-dead-president-orders-investigation-three-recently-abducted-opposition-leaders-remain-missing

¹⁴ BBC News, “Rais wa Tanzania alaan mauaji ya kiongozi wa upinzani kwa kumwagiwa tindikali,” Septemba 9, 2024, bbc.com/news/articles/cqjlnewdzvo

¹⁵ Daily News, “Rais Samia aagiza Polisi kukomesha matukio ya utekaji,” dailynews.co.tz/president-samia-orders-the-police-to-end-abduction-cases

wakidai kwamba wanafamilia walikuwa wamewekwa kando¹⁶, huku mamlaka zikishindwa kuwapa taarifa yoyote kuhusu maendeleo ya uchunguzi.¹⁷

Mauaji bila amri ya mahakama, ya papo hapo au bila ya kufuata utaratibu wa kisheria ni ukiukwaji mkubwa wa haki ya kuishi na utu wa mtu ambayo inalindwa na Ibara ya 4 ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba wa Afrika).

Mnamo Mei 1, 2025, washambuliaji wasiojulikana walimshambuliwa padri wa Kanisa Katoliki, Charles Kitima, Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Tanzania kwenye makao yao yaliyopo kata ya Kurasini Dar es Salaam, saa chache baada ya video yake kusambaa kwa kasi katika mitandao ya kijamii ambapo alikuwa akilaumu kile alichokiita “utendaji kazi usiozingatia sheria” katika jeshi la polisi na kusisitiza haja ya kutenda haki kuelekea uchaguzi wa Tanzania wa mwaka 2025. Kulingana na taarifa ya polisi, shambulio hili lilitokea takribani saa 4:15 usiku wakati Kitima alipokwenda msalani katika mgahawa wa eneo hilo, baada ya kuwa amewasili eneo hilo takribani saa 1:00 usiku. Kitima alipata majeraha makubwa na alilazwa hospitali kwa siku kadhaa. Mnamo Mei 5, 2025, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora – Tanzania (CHRAGG) ililaani shambulio hilo na kutoa wito kwa polisi kufanya uchunguzi wa tukio hilo na kuwatia mbaroni wahasika. Polisi walisema walikuwa wakimshikilia mtu mmoja kuhusiana na tukio hilo, lakini hakuna taarifa mpya kuhusiana na maendeleo ya upelelezi.

Matumizi ya mbinu ya utoweshaji yanakiuka haki kadhaa za msingi chini ya sheria ya kimataifa, ikiwemo Mwongozo kuhusu Ulinzi wa Watu Wote dhidi ya Kutoweshwa barani Afrika, Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Watu Wote dhidi ya Kutoweshwa (2010)¹⁸, na Ibara ya 6 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia ana Kisiasa (ICCPR), ambayo inasema kwamba “kila binadamu ana haki ya asili ya kuishi,” na Ibara ya 9, ambayo inasema kwamba “kila mtu ana haki ya kuwa huru na usalama wa nafsi yake.”¹⁹ Mauaji ya Ali Mohammed Kibao ni ukiukaji wa wazi wa Ibara ya 6 ya ICCPR. Mazingira ya utekaji wake kwenye basi jijini Dar es Salaam ambayo yapo kimaandishi, hatimaye kuteswa kama ushahidi unavyoonesha sura yake kuharibika vibaya kwa kumwagiwa tindikali, na mauaji bila amri ya mahakama yanafanya makossa kadhaa ya ukiukaji mkubwa, ikiwemo kutolewa uhai bila kufuata utaratibu wa kisheria.

Maoni ya Jumla Na. 36 ya Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa yanasisitiza kuwa si tu kwamba serikali hazipaswi kujihusisha na mauaji yasiyofuata utaratibu wa kisheria, lakini lazima pia zichunguze mauaji hayo na kuwafikisha wahasika mbele ya sheria. Mkataba wa Afrika pia unaweka wajibu kwa serikali kuzuia ukatishaji wa maisha bila ya kufuata sheria unaofanywa na mawakala wake, na kuwalinda watu na vikunbdi vya watu dhidi ya ukatishwaji kama huo wakiwa mikononi mwa wengine, na pia kuchunguza mauaji yoyote yanayofanyika na kuwawajibisha wahasika.²⁰ Ukosekanaji wa maendeleo ya uchunguzi, licha ya amri ya rais, unaonesha kushindwa kukidhi wajibu huu chanya.²¹

6. UTESWAJI NA UKATILI MWINGINE

“Ghafa, mtu aliyekuwa amebeba kitu kirefu chenye ncha kali alinichoma upande wa ndani wa kisigino cha mguu wa kushoto, na kunisabishia jeraha kubwa lililokuwa likirusha damu. Kupitia macho yangu ambayo yalikuwa na damu, niligundua kwamba watekaji wangu kadhaa walikuwa wakichukua picha mjongo za tukio, huku wakitucheka na kutukejeli [sisi mateka].”²²

¹⁶ Kauli ya mtoto wa kiume wa Ali Kibao akielezea wasiwasi kuhusu kutokuwepo kwa maendeleo ya uchunguzi wa kifo cha baba yake. X (zamani Twitter), Oktoba 25, 2024, x.com/AliKibao/status/1849742292258639924

¹⁷ Mahojiano kwa njia ya simu kati ya Amnesty International na Mohammed Ali Kibao, mtoto wa mwanamikakati wa upinzani aliyeuawa Ali Mohammed Kibao, Septemba 20, 2024.

²² Mahojiano ya ana kwa ana kati ya Amnesty International na Pendo Jonas Kileo, Aprili 25, 2025.

Mnamo Juni 23, 2024 mwanaharakati wa mtandaoni Edgar "Sativa" Mwakabela, alitekwa takribani saa 7:45 usiku na watu aliowatambua kama askari polisi kutoka eneo la Kimara Korogwe kwenye Barabara ya Maji Chumvi jijini Dar es Salaam. Kulingana na Mwakabela polisi walimpeleka kituo cha polisi cha Oyster Bay cha jijini Dar es Salaam kabla ya kumfunga kitambaa machoni na kumsafirisha kuelekea Arusha na kisha kumtupa katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi, magharibi mwa Tanzania. Utekaji wa Sativa ulifanyika wakati wa maandalizi ya mgomo wa wafanyabiashara wa Kariakoo, eneo kuu la biashara katika jiji la Dar es Salaam, waliokuwa wakilalamikia vitendo vya maafisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ambayo Sativa aliyaandika kwenye mtandao wa X.²³ Licha ya Sativa kuwataja waliohusika katika kumteka, kumsafirisha, na madai ya kumtesa, na kumtekeleza msituni kwenye wanyama wakali, ikiwemo kumtaja Afisa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Kanda ya Dar es Salaam²⁴,

hakuna uchunguzi wa tukio hilo uliofanyika.²⁵ Sativa pia alitaarifu kwamba askari wa polisi waliompeleka msituni pia walimpiga risasi ya kichwa.²⁶



Mnamo Aprili 24, 2025, polisi walijaribu kuwazuia watu wasikusanyike kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kusikiliza mashtaka ya jinai ya uhaini na uchapishaji wa habari za uongo ambayo serikali ilikuwa imemfungulia Lissu. Polisi waliwatia mbaroni makumi ya watu nje ya mahakama. Wengi wa waliokamatwa baadaye walisema walikuwa wamenyanyaswa, wamepigwa, na kufanyiwa vitendo ambavyo vilikuwa sawa na uteswaji au ukatili mwingine, kabla ya kutelekezwa Ununio na Msitu wa Pande, ambao ni pori la akiba la wanyama takribani kilomita 43 kutoka Katikati ya jiji la Dar es Salaam.²⁷ Polisi walimshikilia kwa muda Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, kabla ya kumrudisha kwenye makao makuu ya Chadema yaliyoko Mikocheni jijini Dar es Salaam baadaye usiku siku hiyo.²⁸ Mwanamke mmoja na mwanaume mmoja waliambia Amnesty International kwamba walikuwa wamefanyiwa shambulio la kingono na polisi.²⁹

Mwanaharakati wa mtandaoni Edgar "Sativa" Mwakabela apatikana Hifadhi ya Taifa ya Katavi © Mdude Nyagali

¹⁹ Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu, "Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa," Ibara ya 6 na 9, <https://www.ohchr.org/en/instruments-mechanisms/instruments/international-covenant-civil-and-political-rights>

²⁰ Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, 'Maoni ya Jumla na. 3 kuhusu Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu: Haki ya Kuishi (Ibara ya 4)' Novemba 18, 2015, aya ya 2.

²¹ Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa, "Maoni ya Jumla Na. 36, Ibara ya 6 (Haki ya Kuishi)," <https://docs.un.org/en/CCPR/C/GC/36>

²² Mahojiano ya ana kwa ana kati ya Amnesty International na Pendo Jonas Kileo, Aprili 25, 2025.

²³ Mahojiano ya ana kwa ana kati ya Amnesty International na Edgar 'Sativa' Mwakabela, Oktoba 2024.

²⁴ YouTube, "Sativa Amtuhumu Afande Mafwele Kuratibu Mpango wa Kutekwa Kwake," Imechapishwa Juni 28 2024, www.youtube.com/watch?v=W5110iJ0hgQ

²⁵ The Chanzo, "Taarifa ya Kushtusha: Mtu mwenye miaka 27 Ambaye Alitekwa, Akapigwa Risasi ya Kichwa na Kutupwa Msituni," Juni 28, 2024, thechanzo.com/2024/06/28/shocking-revelation-a-27-year-old-man-who-was-kidnapped-shot-in-the-head-and-dumped-in-the-wild-says-he-was-first-detained-in-a-police-workshop-in-dar

²⁶ Ripoti za kitiba zipo kwenye faili la Amnesty International.

²⁷ Mahojiano ya ana kwa ana kati ya Amnesty International na mashuhuda 23 na wahanga wa ukatili wa polisi, Aprili 25, 2025.

²⁸ Mahojiano ya ana kwa ana kati ya Amnesty International na Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, Aprili 25, 2025.

²⁹ Mahojiano ya ana kwa ana kati ya Amnesty International na wahanga wawili waliodai kufanyiwa shambulio la kingono na polisi, Aprili 25, 2025.

Mnamo Mei 19, 2025, mamlaka za usalama zilimkamata mwanaharakati wa haki a binadamu, Agather Atuhaire, kutoka Uganda, na Boniface Mwangi kutoka Kenya, waliokuwa wamewasili Tanzania Mei 18, 2025 kama sehemu ya ujumbe wa kufutilia kesi ya Tundu Lissu. Baada ya kukamatwa na maafisa wa uhamiaji na polisi kwenye Hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam Mei 19 2025,³⁰ wawili hao walipelekwa kwenye eneo lisilojulikana, ambapo walishikiliwa bila ya kuruhusiwa kuwasiliana na watu wa nje na kutaarifu kwamba walipigwa, waliteswa na kuvuliwa nguo na kuachwa uchi na watu walioaminika kuwa askari wa jeshi la Tanzania. Siku walipokamatwa, Rais Hassan alikuwa ameonya hadharani wanaharakati kutoka nje kutoingilia mambo ya ndani ya Tanzania.³¹ Kwa siku nne, watetezi hao wawili wa haki za binadamu walisema walifanyiwa ukatili. Boniface Mwangi alipatikana akiwa ameteketeleza kwenye kituo cha mpaka wa Kenya na Tanzania Mei 22 wakati Agather Atuhaire aliachwa kwenye mpaka wa Tanzania na Uganda Mei 23. Wote wawili walisafirishwa kila mtu kivyake hadi kwenye vituo vya mpakani na kutupwa huko. Taarifa za kidaktari zilionesha dalili za kuteswa.³² Mnamo Septemba 2025, wakati wa kampeni zake za urais, Rais Hassan alitoa kauli ambazo zinaweza kutafsiriwa kuwa za kutetea matendo ya mamlaka za Tanzania dhidi ya Atuhaire na Mwangi, akisema, “Msiruhusu watu wasio na adabu kutoka nchi nyingine kuvuka mipaka hapa.”³³ Aliendelea kusema kwamba “mamlaka zitawashughulikia wageni hao ipasavyo...”³⁴

Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi (Sura ya 322) inawapa maafisa wa polisi madaraka makubwa lakini haina kinga dhidi ya matumizi mabaya. Kifungu cha 5 kinaelezea shughuli za jumla za Jeshi kama “kulinda amani” na “kuwatia mbaroni na kuwaweka chini ya ulinzi wahalifu” lakini haina taratibu za kutosha za namna ya kukamata watu na kuwaweka kizuizini.³⁵ Kwa Sheria kushindwa kuweka mfumo thabiti wa uwajibikaji kwa mwenendo wa polisi kunatengeneza mazingira wezeshi kwa ukiukwaji tajwa.

Mwongozo na Hatua Zinazokataza na Kuzuia Utesaji, Ukatili, Kutotendewa kwa Utu au Kudhalilishwa au Kuadhibiwa barani Afrika (Mwongozo wa Kisiwa cha Robben au RIG), wa Umoja wa Afrika unafafanua katika Ibara ya 5 ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (Mkataba wa Afrika), ambao unakataza utesaji, ukatili, kutondewa kwa utu na kudhalilishwa au kuadhibiwa (ukatili).³⁶

Ingawa Tanzania haijatia saina kuthibitisha Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Utesaji, Ukatili, Kutotendewa kwa Utu au Kudhalilishwa au Kuadhibiwa (UNCAT)³⁷, katazo la utesaji ni kanuni isiyopingika ya sheria ya kimataifa ambayo hairuhusu msamaha hata kama nchi kihadhi haijasaini mkataba. Aidha, Utesaji unakatazwa katika Katiba yake (Ibara ya 13(6) (e)) (Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977).

7. UTEKWAJI NA UTOWESHWAJI

Kulingana na Mwongozo kuhusu Ulinzi wa Watu Wote Dhidi ya Kutoweshwa barani Afrika, utoweshwaji ni mfululizo wa matendo ya kipekee na yanayohusiana ambayo ni mwendelezo wa ukiukaji wa haki kadhaa za msingi ambazo zipo katika Mkataba wa Afrika, nyingi zikiwa haziwezi kuzuiwa kwa sababu yoyote ile. Orodha ya haki zilizokiukwa, au kuwa na uwezekano wa kukiukwa,

³⁰ Amnesty International, Tanzania: Uteswaji na ufukuzwaji wa wanaharakati wa Kenya na Uganda lazima uchunguzwe haraka, Mei 23, 2025, www.amnesty.org/en/latest/news/2025/05/tanzania-torture-and-forcible-deportation-of-kenyan-and-ugandan-activists-must-be-urgently-investigated/

³¹ WION, Rais Samia wa Awaonya na Kuwafukuza Wanaharakati wa Kenya | World of Africa, Mei 20, 2025, www.youtube.com/watch?v=BwPgQEM6-DD0 “Msiruhusu watu wasio na adabu kutoka nchi nyingine kuvuka mipaka hapa.”

³² Mahojiano kwa njia ya simu na ana kwa ana kati ya Amnesty International na Agather Atuhaire na Boniface Mwangi mwezi Mei na Juni 2025.

³³ The Chanzo, Samia Asisitiza Suala la Amani, Asema Hakutakuwa na Vurugu Siku ya Kupiga Kura, ‘Tumejipanga Vyema, Septemba 20, 2025, www.youtube.com/watch?v=awYtiHOUVAU

³⁴ The Chanzo, Samia Asisitiza Suala la Amani, Asema Hakutakuwa na Vurugu Siku ya Kupiga Kura, ‘Tumejipanga Vyema, Septemba 20, 2025, www.youtube.com/watch?v=awYtiHOUVAU

³⁵ Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi, Sura ya 322, <https://tanzlii.org/akn/tz/act/1939/1/eng@2002-07-31>

³⁶ Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (ACHPR), Kamati ya Kuzuia Utesaji barani Afrika, 2004, achpr.au.int/en/mechanisms/committee-prevention-torture-africa#:~:text=In%20October%202002%2C%20at%20its%2032nd%20Ordinary%20Session%2C,cruel%2C%20inhuman%20or%20degrading%20treatment%20or%20punishment%20%28ill-treatment%29.

³⁷ Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu (OHCHR), Mkataba dhidi ya Utesaji na Ukatili Mwingine, Kutotendewa kwa Utu au Kudhalilishwa au Kuadhibiwa, indicators.ohchr.org/

kutokana na utoweshwaji, haina ukomo. Ingawa tabia hiyo inakiuka haki nyingi, utoweshwaji utachukuliwa kama tendo moja na si muunganiko wa matukio. Kati ya ukukwaji mwingi wa haki, kosa hili la jinai linahusisha wigo mpana wa haki za kiraia na kisiasa, ikiwemo haki ya kuishi; haki ya kutoteswa au kutofanyiwa ukatili mwingine, kukosa utu, na udhalilishaji au adhabu; haki ya kuwa huru na usalama wa mtu; na haki ya kufikishwa mahakamani chini ya mwenendo wa haki wa mashtaka na ulinzi wa taratibu za kuendesha kesi.³⁸

Vikosi vya usalama vya Tanzania vimekuwa vikitumia mfumo wa kufanana wa utoweshwaji unaowalenga wafuasi wa vyama vya upinzani, wanaharakati wa asasi za kiraia, na wakosoaji wa serikali. Wimbi la utekaji wa kimaajabu, ambalo mara nyingi hufuatiwa na kukanusha kupokwa uhuru au kuficha hatma au mahali alipo mhusika, limeendelea licha ya kukemewa hadharani na Rais Hassan, ambaye amelaani waziwazi utoweshwaji na kuagiza vikosi vya ulinzi na usalama kuingilia kati na kukomesha kile alichokiita "wimbi la hofu" linalotisha watu nchini kote. Wahanga wa kupotezwa na kutoweshwa kwa sehemu kubwa ni wakosoaji wa serikali au Rais Hassana, ambao mara nyingi wana ukaribu na vyama vya upinzani, hasa Chadema, au wanaharakati wa haki za binadamu. Wengi wao walilengwa baada kuikosoa serikali kupitia mitandao ya kijamii, hususani X (zamani Twitter).

“Waliokuja kuniteka pale Kimara Korogwe walikuwa watu watatu – wanaume wawili na mwanamke mmoja, kwa mwonekano wao – yule aliyenikaba shingoni alikuwa mrefu na mwenye mwili mkubwa, mkubwa kiasi, ana makovu ...”³⁹



Dioniz Kipanya © Dioniz Kipanya



Deusededith Soka © Deusededith Soka

Mnano Julai 26, 2024, Dioniz Kipanya, afisa wa Chadema, alipotea baada ya kuondoka nyumbani kufuatia mazungumzo ya simu na mtu asiyejulikana.⁴⁰ Hadi taarifa hii inatolewa alikuwa bado hajapatikana.⁴¹ Mnamo Agosti 18, 2024, Deusededith Soka na Jacob Mlay wote wakiwa wanaharakati vijana wa Chadema, na Frank Mbise, mwendesha bodaboda walichukuliwa na kundi la watu katika wilaya ya Temeke, Dar es Salaam.⁴² Soka alikuwa mstari wa mbele kuhamasisha wimbi la mabadiliko ya kisiasa nchini Tanzania na alitoweka siku chache baada ya kutangaza dhamira yake ya kuongoza maandamano ya vijana nchi nzima kudai mabadiliko hayo.⁴³

³⁸ Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (ACHPR), Mwongozo kuhusu Ulinzi wa Watu Wote dhidi ya Kutoweshwa barani Afrika, sehemu ya 3: hakia ambazo kwa kwaida hukiukwa wakati wa kutoweshwa

³⁹ Mahojiano kwa njia ya simu kati ya Amnesty International na Edgar Mwakabela, Septemba 2025.

⁴⁰ Amnesty International, Tanzania: Acha kukandamiza viongozi wa upinzani na mwachie mara moja Tundu Lissu, Aprili 11, 2025, www.amnesty.org/en/latest/news/2025/04/tanzania-stop-repression-of-opposition-leaders-and-immediately-release-tundu-lissu/

⁴¹ Amnesty International, Tanzania: Acha kukandamiza viongozi wa upinzani na mwachie mara moja Tundu Lissu, Aprili 11, 2025, www.amnesty.org/en/latest/news/2025/04/tanzania-stop-repression-of-opposition-leaders-and-immediately-release-tundu-lissu/

⁴² Amnesty International, Tanzania: Acha kukandamiza viongozi wa upinzani na mwachie mara moja Tundu Lissu, Aprili 11, 2025, www.amnesty.org/en/latest/news/2025/04/tanzania-stop-repression-of-opposition-leaders-and-immediately-release-tundu-lissu/

⁴³ The Chanzo, “Mwaka Mmoja Baadaye: CHADEMA Yamkumbuka Deusededith Soka Ingawa Bado Hajulikani Alipo,” Agosti 18, 2025, thechanzo.com/2025/08/18/one-year-on-chadema-honors-deusededith-soka-amid-unsolved-disappearance

Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS) kilitangaza idadi ya watu 83 waliopotea katika mazingira ya kutatanisha hadi kufikia Agosti 9, 2024.⁴⁴ Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), taasisi ya haki za binadamu nchini ilisema mnamo Agosti 22, 2024, kwamba ilikuwa ikifanya uchunguzi maalum kuhusu matukio hayo, lakini umma haujulishwa iwapo uchunguzi huo umekamilika au ikiwa ripoti itawekwa hadharani.⁴⁵

Mnamo Desemba 1, 2024, Abdul Nondo, mwenyekiti wa tawi la vijana la ACT Wazalendo, alitoa taarifa kwamba aliteka kwenye kituo cha daladala jijini Dar es Salaam saa 11:00 alfajiri wakati akirejea kutoka Kigoma. Aliachiwa saa 18 baadaye baada ya kutelekezwa kwenye ufukwe wa Coco Beach jijini Dar es Salaam eneo la Oyster Bay, akiwa na majeraha na alipatiwa matibabu katika hospitali ya Aga Khan jijini Dar es Salaam.⁴⁶

Mnamo Machi 23, 2025, Daniel Chonchorio, mwanachama wa CCM na mfanyabiashara wa jijini Mwanza, alipotea na hadi sasa hajapatikana. Wanachama wawili waliokuwa wakishiriki katika kura za maoni ndani ya CCM kwa wagombea wa ubunge na udiwani wameripotiwa kupotea katika mazingira ya kutatanisha: Sinda Mseti, aliyekuwa akigombea katika kura za maoni kwa ngazi ya udiwani katika Kata ya Sirari, Tarime, alitoweka Agosti 6, 2025; na Siza Mwita Keheta, aliyekuwa akigombea katika Kata ya Ganyange, Tarime, alitoweka Julai 29, 2025. Aidha Anthony Gabriel, rafiki wa mmoja wa wagombea waliotoweka, naye pia aliripotiwa kutoweka.⁴⁷

Mnamo Aprili 2, 2025, ACT Wazalendo ilitaarifu kutekwa kwa mwanachama wake, Fakihi Ali Salim, mkazi wa Wete, Pemba Kaskazini, ambaye alitoweka mnamo Machi 27, 2025, takribani saa 11:00 alfajiri. Hadi leo hajapatikana. Kulingana na familia yake, kitendo cha mwisho kinachojulikana kilihusisha kutekeleza ombi kutoka kwa mpiga simu ambaye hakujulikana la kumuuzia kuku. Alionekana akiingia katika gari la Harrier katika Kijiji cha Minyenyezi saa 11:00 alfajiri.⁴⁸



Mdude Nyagali © Mdude Nyagali

Mnamo Mei 2, 2025, washambuliaji wasiojulikana walivamia nyumbani kwa Mdude Nyagali, kada wa Chadema na mkosoaji mkubwa wa serikali ya Rais Hassan na kumteka. Washambuliaji hao walimpiga vibaya, wakiacha damu ikiwa imetapakaa kwenye varanda ya nyumba yake, kabla ya kumteka. Maafisa wawili wa polisi walidaiwa kushiriki katika tukio hilo, huku jeshi la polisi likitoa ahadi ya kufanya uchunguzi wa tuhuma hizo ili kuthibitisha ukweli. Hata hivyo, polisi baadaye walikanusha tuhuma hizo, wakisema kwamba askari wao hawakuhusika katika tukio hilo.⁴⁹ Msemaji wa Polisi David Misime alitoa taarifa mnamo Juni 18, 2025, akikitenga chombo hicho cha sheria na uhusikaji wowote katika tukio hilo. Alisema kwamba uchunguzi kuhusu matukio kadhaa ya kutekwa

⁴⁴ Chama cha Wanasheria wa Tanganyika, "Ongezeko la Vitendo vya Utekaji na Upoteaji wa Watu Nchini," Agosti 8, 2024 (kwenye faili la Amnesty International).

⁴⁵ Kamishna wa Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG)/THBUB, "THBUB Yatoa Tamko Kuhusu Kupotea Kwa Watu Nchini," Agosti 8, 2024 (kwenye faili la Amnesty International).

⁴⁶ The Chanzo, "ACT Wazalendo Imesema Kiongozi wake wa tawi la Vijana, Abdul Nondo, Ametekwa," Desemba 1, 2024,

thechanzo.com/2024/12/01/act-wazalendo-says-its-youth-wing-leader-abdul-nondo-has-been-abducted/

⁴⁷ Mwananchi, "Familia yaomba kinara kura za udiwani aliyetoweka Sirari arejeshwe," Agosti 8, 2025, mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/familia-yaomba-kinara-kura-za-udiwani-aliyetoweka-sirari-arejeshwe-5148184

⁴⁸ The Chanzo, "ACT Wazalendo Yadai Mwanachama Wake Kutekwa Pemba, Aprili 2, 2025, thechanzo.com/2025/04/02/act-wazalendo-yadai-mwanachama-wake-kutekwa-pemba

⁴⁹ The Chanzo, "Mwaka Mmoja Baadaye: CHADEMA Yamkumbuka Deusedith Soka Ingawa Bado Hajulikani Alipo," Agosti 18, 2025, thechanzo.com/2025/08/18/one-year-on-chadema-honors-deusedith-soka-amid-unsolved-disappearance/

ulikuwa umeibua mlolongo wa kusikitisha, akihitimisha kwamba wengi wa watu ambao wametolewa taarifa ya kupotea, walikuwa wamesingizia kujiteka wao wenyewe.

Mnamo Oktoba 6, 2025, washambuliaji wasiojulikana walimteka balozi wa zamani wa Tanzania nchini Cuba Humphrey Polepole. Kulingana na familia yake, walikuwa wamepewa tahadhari ya uwezekano wa tukio la kuvunjwa na kuingia katika makazi ya mwanadiplomasia huyo na mkosoaji mkubwa wa serikali. Walipofika hapo, walikuta mlango umevunjwa, nyaya za umeme zikiwa zimekatwa, na kiasi kikubwa cha damu kwenye eneo la tukio. Video na picha zilizotolewa na familia zinaonekana kuthibitisha madai hayo, zikionesha dalili za wazi za makabiliano ya nguvu.⁵⁰ Familia ya Polepole iliripoti tukio hilo katika Kituo cha Polisi cha Mbezi mnamo Oktoba 6, na wakili wake alifungua ombi dogo mahakamani la kuitaka serikali ioneshe mahali alipo (Habeas corpus) mnamo Oktoba 7, 2025.⁵¹ Msemaji wa polisi David Misime alieleza kwamba Polepole alikuwa amepolekewa wito wa kufika katika ofisi ya Mkurugenzi wa Uchunguzi wa Mashtaka ya Jinai (DCI) kuhusu madai aliyokuwa ameyatoa kupitia mitandao ya kijamii lakini alishindwa kuitikia.

Sheria ya Uchaguzi ya Taifa (Sura ya 343) haina vifungu mahsusi vinavyozungumzia kulinda wanasiasa dhidi ya utoweshwaji, licha ya ulengaji wa dhahiri wa wanasiasa wa upinzani ulioainishwa katika kesi za Kibao, Soka, Mlay, Mbise, na Nyagali.⁵² Pengo hili la kisheria linafifisha ubora wa mchakato wa uchaguzi na kukiuka Ibara ya 25 ya ICCPR, ambayo inalinda haki ya kushiriki shughuli za umma.⁵³ Utoweshwaji ni ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu, ikiwemo haki ya kuishi, uhuru na usalama wa watu unaolindwa chini ya sheria ya kimataifa kuhusu haki za binadamu.

Mbali ya haki za kiraia na kisiasa, pia kuna athari za kiuchumi, kijamii, na za haki za kiutamaduni, kama vile haki ya kuwa na afya njema, haki ya kuwa na maisha ya kifamilia, na haki ya kupata elimu, kati ya nyingi nyinginezo. Pamoja na kukiuka haki za binadamu, utoweshwaji unakiuka kanuni nyingi za kimila na kimkataba za haki za binadamu za kimataifa na sheria za ubinadamu (IHL), kubwa kabisa ikiwa katazo la kunyimwa uhuru bila ya kufuata taratibu za kisheria, utesaji, na matendo mengine ya kikatili au yasiyokuwa ya utu, na mauaji, kama ilivyoelezewa katika Utafiti wa Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu (ICRC) kuhusu Sheria ya Kimila kuhusu Utu Kimataifa.⁵⁴ Kulingana na Kikosi Kazi cha Umoja wa Mataifa kuhusu Kutoweshwa au Kupotezwa Bila Hiari (WGEID), kosa hili la jinai linatambulika kama ukiukwaji unaoendelea, ukiongeza hatari yake na uhitaji wa kulishughulikia kabisa kisheria na kibinadamu.⁵⁵

8. UWEKWAJI KIZUIZINI BILA KUFUATA TARATIBU ZA KISHERIA NA MASHTAKA YASIYOZINGATIA SHERIA

Ibara ya 9 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kisiasa na Kiraia (ICCPR) inakataza kukamatwa au kuwekwa kizuizini bila ya kufuata sheria. Maoni ya Jumla Na. 35 ya Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa yanaelezea zaidi mazingira mengine kadhaa ambayo kwayo kukamatwa kwa mtu kunaweza kuwa kinyume cha sheria. Kadhalika, “kuwekwa kizuizini bila utaratibu ni pale ambapo serikali itashindwa kutoa sababu ya kisheria au utaratibu wa kutosha wa mchakato wa kisheria.” Katika hali kama hiyo, uwekwaji kizuizini kunakosa uhalali chini ya viwango vya sheria vya kitaifa na kimataifa na hivyo basi inachukuliwa kuwa ni kuwekwa kizuini bila ya kufuata sheria.⁵⁶

⁵⁰ Mahojiano kwa njia ya simu kati ya Amnesty International na Augustino Polepole, kaka yake Humphrey Polepole mnamo Oktoba 7, 2025.

⁵¹ Mahojiano kwa njia ya simu kati ya Amnesty International na Peter Kibatala na Tito Magoti, mawakili wa Humphrey Polepole, Oktoba 7, 2025.

⁵² Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343, <https://tanzlii.org/akn/tz/act/1985/1/eng@2010-08-06>

⁵³ Mkataba wa Kimataifa kuhusu haki za Kiraia na Kisiasa, Ibadra ya 25, <https://www.ohchr.org/en/instruments-mechanisms/instruments/international-covenant-civil-and-political-rights>

⁵⁴ Jean-Marie Henckaerts and Louise Doswald-Beck, Customary International Humanitarian Law, Volume I: Rules, International Committee of the Red Cross (ICRC), Cambridge University Press, 2005.

⁵⁵ Kikosi Kazi cha Umoja wa Mataifa kuhusu Kutoweshwa au Kupotezwa Bila Hiari (WGEID), Maoni ya Jumla kuhusu Utoweshwaji kama Uhalifu Unaokomaa, A/HRC/16/48 (Januari 26, 2011), aya ya 39.

⁵⁶ Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu (OHCHR), Maelezo Muhimu Na. 26 (Rev. 1): Kikosi Kazi kuhusu Kuwekwa Kizuizini Bila Kufuata Taratibu za Kisheria, Februari 14, 2024, www.ohchr.org/en/publications/fact-sheets/fact-sheet-no-26-rev-1-working-group-arbitrary-detention

Baada ya mtu kushikiliwa, ana haki ya kumwona mwanasheria na wanafamilia. Wanaonyimwa haki hiyo wanakuwa wamewekwa kizuizini bila haki ya kufanya mawasiliano. Katika matukio mengine, pamoja na kunyimwa kufanya mawasiliano na watu wa nje, wafungwa au watu waliowekwa kizuizini wanakuwa wameshikiliwa katika maeneo yanayofahamika kwa mamlaka tu – hii inafahamika kama kuwekwa kizuizini kwa siri na inaweza kuwa sawa na kutoweshwa.⁵⁷

Mnamo Aprili 9, 2025, polisi walimkamata Tundu Lissu baada ya kufanya mkutano wa kisiasa mjini Mbinga, kusini magharibi mwa Tanzania. Baada ya hapo aliamishwa Dar es Salaam, umbali wa zaidi ya kilomita 1,000 kwa barabara wakati wa usiku. Polisi walitumia nguvu kupita kiasi na ambayo haikuwa lazima wakati wa kumkamata, ikiwemo kupiga mabomu ya machozi na kurusha risasi hewani kutawanya wafuasi wake waliokuwa wamemzunguka wakati wa kukamatwa kwake.⁵⁸

“Mahakama ya Kisutu [jijini Dar es Salaam] haikuwa na mamlaka kisheria ya kusikiliza kesi yangu. Ilipaswa nishtakiwe Mbinga, nilipokamatiwa. Hii ni kinyume cha sheria. Nimewekwa kizuizini bila ya sababu zozote za kisheria.”⁵⁹

Mnamo Aprili 10, 2025, polisi walimfungulia mashtaka ya uhaini, kosa ambalo halina dhamana, kuhusiana na kauli alizozitoa wakati wa mkutano na waandishi wa habari mnamo Aprili 4, 2025 jijini Dar es. Maneno halisi ambayo yanatengeza sababu za mashtaka ni: “Wamesema jambo moja sahihi hapo, wanasema msimamo huu unaashiria uasi, ni kweli. Kwa sababu tunasema tutazuia uchaguzi, tutahamasisha uasi, hiyo ndiyo njia ya kuleta mabadiliko, hiyo ndiyo njia ya kuleta mabadiliko.”⁶⁰ Tundu Lissu alitoa wito kwa Watanzania kususia uchaguzi ujao, akitoa uwezekano wa kuibwa kwa kura.⁶¹ Serikali pia ilimfungulia mashtaka matatu kuhusiana na “kuchapisha taarifa potofu” kwa kutumia sheria ya makosa ya kimtandao. Mnamo Aprili 3, 2025, Tundu Lissu, katika chapisho la YouTube alisema pia kwamba polisi wa Tanzania walishiriki katika kile alichodai kuwa ukiukwaji wa maadili ya uchaguzi ambao alidai uliamriwa na rais kufuatia uchaguzi wa serikali za mtaa wa Novemba. Pia alisema kwamba majaji nchini hawakuwa na uhuru na walikuwa wakipata shinikizo kutoka chama tawala.⁶²

⁵⁷ Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa (HRC), Maoni ya Jumla Na. 35, Ibara ya 9 (Uhuru na Usalama wa Mtu), CCPR/C/GC/35, Desemba 16, 2014.

⁵⁸ Amnesty International, Tanzania: Acha kukandamiza viongozi wa upinzani na mwachie mara moja Tundu Lissu, Aprili 11, 2025, www.amnesty.org/en/latest/news/2025/04/tanzania-stop-repression-of-opposition-leaders-and-immediately-release-tundu-lissu/

⁵⁹ Tundu Lissu mahakamni Septemba 2025, “Mahakama ya Kisutu haikuwa na mamlaka yoyote. Nilipaswa kushtakiwa Mbinga, ambako nilikamatwa. Hii ni kinyume cha sheria. Nimewekwa kizuizini bila msingi wa kisheria.”

⁶⁰ “Wamesema kitu kimoja sahihi hapo, wanasema msimamo huu unaashiria uasi, ni kweli. Kwa sababu tunasema tunazuia uchaguzi, tutahamasisha uasi, hiyo ndiyo namna ya kupata mabadiliko, ndiyo namna ya kupata mabadiliko. Mandela had to go through life in prison for treason ili kupata mabadiliko Afrika Kusini. Kwahiyo tunaenda kucinukisha, walio tayari tutakwenda nao, hakuna mtu atawekwa bunduki kwenda... kama unataka kuwa mbunge seriously twende tukapiganie mabadiliko... huuu uchaguzi tutauvuruga, kama ulikuwa unafikiria kuwa Mbunge Oktoba au Novemba sahai... mimi nimekinukisha, ninakamatwa... ninakwenda kushitakiwa kwa uhaini kwa kuhamasisha uasi.”

⁶¹ Amnesty International, Tanzania: Acha kukandamiza viongozi wa upinzani na mwachie mara moja Tundu Lissu, Aprili 11, 2025, www.amnesty.org/en/latest/news/2025/04/tanzania-stop-repression-of-opposition-leaders-and-immediately-release-tundu-lissu/

⁶² Amnesty International, Tanzania: Acha kukandamiza viongozi wa upinzani na mwachie mara moja Tundu Lissu, Aprili 11, 2025, www.amnesty.org/en/latest/news/2025/04/tanzania-stop-repression-of-opposition-leaders-and-immediately-release-tundu-lissu/



Tundu Lissu katika Mahakama Kuu ya Tanzania jijini Dar Es Salaam, Agosti 2025 © CHADEMA

Tangu kukamatwa kwake, Lissu amebakia rumande kwa sababu shtaka lake la uhaini halina dhamana. Lissu alikubaliwa Juni 23, 2025 kujiwakilisha mwenyewe katika kesi ya uhaini dhidi yake baada ya kunyimwa haki ya kukutana na mawakili wake kwa faragha na uongozi wa magereza.⁶³

Mnamo Julai 23, 2025, mamlaka za usalama za Tanzania zilimteka mwanaharakati wa haki za binadamu kutoka Kenya Mwabili Mwagodi nchini Tanzania. Mwagodi, ambaye anafahamika kwa ukosoaji wake kuhusu taasisi za dini kuingiliwa na mashinikizo ya kisiasa na uhamasishaji wake wa makundi ya vijana huko Kenya, alionekana mara ya mwisho akiwa Dar es Salaam ambapo alikuwa akifanya kazi na kampuni ya utalii. Mashuhuda walithibitisha kwamba alichukuliwa na watu wasiojulikana kwenye pikipiki.⁶⁴ Mwagodi alitupwa kichakani huko Kinondo, kaunti ya Kwale, kwenye pwani ya Kenya takribani saa tisa usiku Julai 27, 2025, ambapo alitembea takribani kilomita tatu hadi kituo cha polisi cha Diani ambapo aliomba msaada, ikiwemo msaada wa matibabu. Kulingana na Mwagodi, mamlaka za Tanzania zilichukua simu yake, kompyuta mpakato yake, na kumhoji kuhusu maandamano na maslahi ya kisiasa.⁶⁵

9. UKIUKWAJI WA HAKI YA KUKUSANYIKA KWA AMANI

“Kila mtu ana haki ya kukusanyika kwa uhuru na watu wengine. [...]”⁶⁶

Mamlaka za Tanzania mara kwa mara zimepiga marufuku, zimevuruga, au kutawanya kwa nguvu makusanyiko ya amani, hasa yale yanayoandaliwa na vyama vya upinzani.

⁶³ Mahojiano kwa njia ya simu kati ya Amnesty International na mawakili wanne wanaomwakilisha Tundu Lissu, Septemba 2025.

⁶⁴ Julai 26, 2025, www.amnestykenya.org/amnesty-international-statement-on-the-reported-abduction-of-kenyan-activist-mwabili-mwagodi/

⁶⁵ Mahojiano kwa njia ya simu kati ya Amnesty International na mashuhuda watatu waliomwona Mwagodi huko Diani, akiwemo dada yake, wanaharakati wa haki za binadamu, na Mwagodi mwenyewe, Julai 2025.

⁶⁶ Ibara ya 11 ya Mkataba wa Afrika

Mnamo Julai 21, 2024, polisi walimtia mbaroni kiongozi wa upinzani Freeman Mbowe na maafisa wengine 11 wa Chadema pamoja na wafanyakazi katika hoteli jijini Mwanza, kaskazini magharibi mwa Tanzania. Walikamatwa saa chache kabla ya kufanya mkutano uliokuwa umepangwa, ambao wanachama wangejadili kudai Katiba mpya ya nchi. Ingawa saba kati yao waliachiwa siku kadhaa baada ya kutia mbaroni, Mbowe aliachiwa baada ya zaidi ya miezi saba baadaye, baada ya mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai kufuta mashtaka ya ughaidi dhidi yake na watu wengine watatu.⁶⁷

Mnamo Agosti 11, 2024, polisi wa Tanzania waliwatia mbaroni na kuwaweka rumande viongozi waandamizi wa Chadema wakiwemo Tundu Lissu, John Mnyika, kiongozi wa Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi, viongozi wa jumuiya ya vijana ya chama, Baraza la Vijana la Chadema (Bavicha) na zaidi ya vijana mia moja wa chama, pamoja na waandishi wa habari watano kwa kukaidi katazo la kufanya mkutano wa vijana. Walikamatwa kwenye mkutano wa Chadema kwenye ofisi za kanda ya Nyasa jijini Mbeya, kusini magharibi mwa Tanzania, kama sehemu ya maandalizi ya Siku ya Vijana Kimataifa Agosti 12, 2024.⁶⁸ Kulingana na afisa mmoja wa chama, viongozi hao waandamizi walipelekwa na polisi sehemu zisizojulikana, wakati wanachama wengine na waandishi wa habari walipelekwa kwenye vituo mbalimbali vya polisi vya Mbeya. Polisi baadaye, mnamo Agosti 12, 2024, walimkamata aliyekuwa mwenyekiti wa Chadema Freeman Mbowe na kiongozi wa Bavicha kitaifa John Pambalu kwenye uwanja wa ndege wa Songwe baada ya kuwasili kutokea Dar es Salaam kufuatilia hatma ya viongozi wa chama na wanachama wengine waliokuwa wamekamatwa.⁶⁹

Mnamo Aprili 23, 2025, polisi wa Dar es Salaam waliwakamata viongozi kadhaa wa chama, akiwemo John Heche, Makamu Mwenyekiti (Tanzania Bara), ili kuzuia maandamano ambayo chama kilikuwa kimepanga kufanya katika eneo la Kariakoo. Katika barua yao ya Aprili 22, 2025, polisi walisema walikuwa wamekataza mkutano huo ili kuepuka kuvuruga shughuli za biashara katika eneo la soko kuu la Dar es Salaam.⁷⁰ Siku iliyofuata, Aprili 24, 2025, polisi waliwapiga na kuwatia mbaroni watu waliokuwa wamekusanyika kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kusikiliza kesi dhidi ya Lissu.⁷¹

“Tulipokaribia mahakamani, niliona uwepo wa polisi wengi ambao haukuwa wa kawaida yakiwemo magari ya kivita yakiwa yameegeshwa kuzunguka lango kuu. Hata kwenye eneo la mahakama, kulikuwa na askari polisi, wa Kikosi cha Kuzuia Fujo (FFU) na walituzuia kuingia mahakamani. Kwa hiyo, tuliamua kusimama nje na kufuatilia kesi kutokea hapo wakati tukifikiria nini cha kufanya.”⁷²

⁶⁷ Amnesty International, Tanzania: Komesha ukamataji zoazoa na kuwazuia kiholela wapinzani wa kisiasa, Agosti 12, 2024, www.amnesty.org/en/latest/news/2024/08/tanzania-end-mass-arrests-and-arbitrary-detentions-of-political-opposition/

⁶⁸ Amnesty International, Tanzania: Komesha ukamataji zoazoa na kuwazuia kiholela wapinzani wa kisiasa, Agosti 12, 2024, www.amnesty.org/en/latest/news/2024/08/tanzania-end-mass-arrests-and-arbitrary-detentions-of-political-opposition/

⁶⁹ Amnesty International, Tanzania: Komesha ukamataji zoazoa na kuwazuia kiholela wapinzani wa kisiasa, Agosti 12, 2024, www.amnesty.org/en/latest/news/2024/08/tanzania-end-mass-arrests-and-arbitrary-detentions-of-political-opposition/

⁷⁰ Jeshi la Polisi Tanzania, barua kwenda CHADEMA ikikataza mkutano eneo la Kariakoo, Aprili 22, 2025, (kwenye faili la Amnesty International).

⁷¹ Mahojiano ya Amnesty International, Dar es Salaam, Aprili 25, 2025. Mahojiano kwa njia ya simu na ana kwa ana yaliyofanywa na maafisa wa Chadema na wanachama 23 ambao walikamatwa na polisi mnamo Aprili 24 na baadaye kuachiwa.

⁷² Mahojiano kwa njia ya simu na ana kwa ana kati ya Amnesty International na maafisa wa Chadema party jijini Dar es Salaam, Aprili 25, 2025.



Mnamo Juni 2, 2025, Wizara ya Mambo ya Ndani kwa njia ya barua ilifuta leseni ya Kanisa la Ufufuo na Uzima Tanzania (Glory of Christ Tanzania Church), linaongozwa na mkosoaji wa serikali, Askofu Josephat Gwajima ambao pia ni Mbunge wa Kawe kwa chama tawala, CCM.⁷³ Katika barua hiyo kwenda kwa Gwajima kutoka kwa Msajili wa Asasi za Kiraia, mamlaka ilidai kwamba kanisa hilo lilikuwa limevunja sheria kwa kuchanganya siasa na dini, ikieleza kwamba mahubiri yake yalikuwa “yakihamasisha chuki ya wananchi dhidi ya serikali” na “kutishia usalama na utulivu” kinyume na kifungu cha 17 na 39 cha Sheria ya Asasi za Kiraia.⁷⁴

Gwajima alikuwa amezitaka hadharani mamlaka kuchukua hatua kukomesha matukio ya kutoweshwa kwa wakosoaji wa serikali, akimlaumu Rais Hassan. Waumini wa Kanisa la Ufufuo na Uzima Tanzania wamekuwa wakipata taabu kukusanyika kwa ajili ya kufanya ibada, huku polisi wakiwatawanya kwa nguvu kila Jumapili pale waumini wanapokutana, wakati mwingine kwa kutumia maji ya kuwasha.⁷⁵

Tukio la kukamatwa kwa viongozi kadhaa wa chama, akiwemo John Heche, Naibu Mwenyekiti wa Chadema jijini Dar Es Salaam, Agosti 23, 2025 © CHADEMA

Mnamo Juni 10, 2025, Mahakama Kuu Dar es Salaam ilitoa zuio kwa Chadema kufanya shughuli zozote za kisiasa. Amri hii ilitokana na kesi ambayo ilidai kuwepo kwa tofauti kwa namna ambavyo chama kinatoa rasilimali kati ya Tanzania bara na visiwa vya Zanzibar ambavyo vina madaraka ya ndani.⁷⁶ Zuio hilo limeathiri vibaya ukusanyikaji kwa amani wa wanachama na mashabiki wengi wa Chadema nchi nzima.

Mnamo Septemba 8, 2025, makumi ya mashabiki wa Chadema walitiwa mbaroni na polisi kwa kufanya kile polisi walichokiitia “mikusanyiko haramu.” Septemba 7, 2025, polisi waliwazuia wanachama na mashabiki kukusanyika ili kuadhimisha “*Siku ya Mashujaa*”, tukio ambalo Chadema walikuwa wameliandaa kwa kumbukumbu ya waliopotexa maisha wakipigania demokrasia Tanzania. Huko Serengeti, Mkoa wa Mara, polisi waliwatia mbaroni viongozi kadhaa waandamizi wa Chadema wakati walipokuwa wakifanya usafi kwenye kaburi la Bob Makani, mmoja wa waasisi wa chama, na kuitembelea familia yake. Siku hiyo hiyo, jijini Mwanza, kaskazini magharibi mwa Tanzania, polisi waliwatia mbaroni zaidi ya watu 20 waliokuwa wamekusanyika kanisani kuadhimisha *Siku ya Mashujaa*.⁷⁷ Amnesty International ilithibitisha kupitia mahojiano na msemaji wa chama kwamba hakuna mashtaka yaliyokuwa yamefunguliwa dhidi ya yeyote kati yao. Jijini Dar es Salaam, polisi walizingira ofisi za Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS) kuzuia kufanyika kwa tukio kama hilo lililokuwa limepangwa la kuadhimisha *Siku ya Mashujaa*.⁷⁸

⁷³ Serikali ya Tanzania, taarifa kwenye Instagram, Septemba 24, 2025, www.instagram.com/p/DKZqQkMPxt1/

⁷⁴ Barua kutoka kwa Msajili wa Asasi za Kiraia, Emmanuel Kihampa ya Juni 2, 2025 (kwenye faili la Amnesty International).

⁷⁵ Josephat Gwajima, taarifa kwenye YouTube, Septemba 23, 2025, www.youtube.com/watch?v=NhpB9Zh2_6Y

⁷⁶ Mahakama Kuu ya Tanzania, *Mwanasheria Mkuu wa Serikali v. CHADEMA, Miscellaneous Civil Application No. 2987 of 2025*, Juni 10, 2025 (kwenye faili la Amnesty International).

⁷⁷ Chadema, taarifa kwenye X, Septemba 25, 2025, x.com/ChademaTZ/status/1964641556369215673

⁷⁸ Mahojiano kwa njia ya simu kati ya Amnesty International na Amani Golugwa, Septemba 2025.

Sheria ya Ulinzi wa Amani (The Public Order Act), ambayo polisi waliitumia katika hatua zao dhidi ya Chadema, inatoa mamlaka mapana kwa polisi kuyatumia kama wapendevyo kudhibiti makusanyiko lakini haina inakosa mwongozo wa namna ya matumizi yake.⁷⁹ Kifungu cha 5 cha Sheria ya Kutunza Amani inataja kuwa ni kosa la jinai mwenendo ambao “unatishia, kuhatarisha, or kutukana, na au unaolenga kusababisha uvunjifu wa amani au kuwa na uwezekano wa kufanya hivyo.” Kiutendaji, mamlaka zimetumia kipengele hicho kwa mtazamo binafsi—hasa katika kutafsiri maneno kama vile “kutishia” au “uwezekano wa kusababisha”—jambo linalowapa polisi wigo mpana wa kuingilia mikusanyiko ya umma.

Ikitumiwa pamoja na Sheria ya Vyama vya Siasa (Sura ya 258), 2019, ambayo inaelekeza utaratibu wa utendaji kazi wa shughuli za vyama vya siasa, sheria hizo mbili zina vipengele ambavyo vimekuwa vikitumika kufinyia shughuli halali za vyama vya siasa. Lugha ya madaraka makubwa iliyotumika katika Sheria ya Vyama vya Siasa kuhusu shughuli zinazotishia “umoja wa kitaifa” au “utulivu wa umma” haitoi mwongozo wa kutosha wa matumizi yanayofanana na inatoa mwanya wa utekelezaji wa kibaguzi.⁸⁰

Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi inawataka waandaaji wa mkutano kutoa taarifa polisi saa 48 kabla ya kufanyika kwa kusanyiko lolote lile la umma. Polisi wanayo hiari ya kutotoa kibali ikiwa mkutano utadhaniwa kuwa na uwezekano wa uvunjifu wa amani au utulivu wa umma.⁸¹

Ibara ya 11 ya Mkataba wa Afrika inalinda “haki ya kukusanyika kwa uhuru na watu wengine. Matumizi ya haki hii yatazuiwa tu na makatazo ya lazima yaliyoanishwa kisheria, hususani yale yaliyopitishwa kisheria kwa maslahi ya usalama wa taifa, usalama, afya, maadili na haki na uhuru wa watu wengine.”⁸² Mnamo Mei 2017, Tume ya Afrika ilitoa Mwongozo kuhusu Uhuru wa Kujumuika na Kukusanyika wa Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu. Mwongozo huo unaelekeza namna ambavyo nchi wanachama lazima ziwe na utaratibu kisheria wa wazi na dhahiri wa kupata uhuru wa kukusanyika kwa amani ambao unatambulika katika katiba na/au sheria za nchi.⁸³

Kuzuia kinfumo kukusanyika kwa amani kunakiuka Ibara ya 21 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) na Ibara ya 20 ya Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR) ambayo inasema kwamba “haki ya kukusanyika kwa amani itambuliwe.”⁸⁴

10. USHAMBULIWAJI WA UHURU WA KUJIELEZA NA VYOMBO VYA HABARI

“Tumeanza kuona mtindo wa wanaharakati kutoka ukanda wetu kuja kuingilia mambo yetu. Kama tayari wamekwishaadhibiwa kwao, wasije hapa kutuharibia. Tusitoe nafasi...”⁸⁵

Polisi waliwatia mbaroni na kuwashikilia wanasiasa wa upinzani kwa kauli walizozitoa kwenye majukwaa ya kisiasa, hususani zile zilizomhusu Rais Hassan. Uhuru wa habari na uwezo wa watu kutoa maoni yao kwa uhuru umefinywa kwa kiwango kikubwa sana wakati Tanzania inapoelekea

⁷⁹ Sheria ya Ulinzi wa Umma, imerejelewa katika vitendo vya polisi dhidi ya mikutano ya CHADEMA

⁸⁰ Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258, <https://tanzlii.org/akn/tz/act/1992/5/eng@2019-11-30>

⁸¹ Kifungu cha 43 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi (Sura ya 322).

⁸² Ibara ya 11 ya Mkataba wa Afrika.

⁸³ Amnesty International, Mwongozo kuhusu haki ya uhuru wa kukusanyika kwa amani, Novemba 27, 2024, www.amnesty.org/en/documents/act30/8426/2024/en/

⁸⁴ Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, “Mkataba wa Kimataifa kuhusu haki za Kiraia na Kisiasa,” Ibara ya 21, <https://www.ohchr.org/en/instruments-mechanisms/instruments/international-covenant-civil-and-political-rights>

⁸⁵ Citizen TV, Rais Samia awaonya wanaharakati wa kigeni kukaa mbali, Mei 19, 2025, www.bing.com/videos/riverview/relatedvideo?q=Samia%20Suluhu%20September%202025%20akisema%20aliwadhabit%20wagani&mid=4CC82223F880C37CF8324CC82223F880C37CF832&ajaxhist=0

“Tumeanza kuona mtindo wa wanaharakati kutoka ukanda wetu kuja kuingilia mambo yetu. Kama tayari wamekwishaadhibiwa kwao, wasije hapa kutuharibia. Tusitoe nafasi—tayari wameleta vurugu kwao ...” (unofficial translation from Kiswahili to English).

katika uchaguzi mkuu, jambo linalotishia kudhoofisha uwezo wa umma kupata habari inayohitajika ili kushiriki kikamilifu katika mchakato wa uchaguzi.

Mnamo Julai 2024, Mahakama ya Mwanzo ya Rungwe, Mbeya, kusini magharibi mwa Tanzania, ilimhukumu mchoraji na mwanamtandao wa TikTok, Shadrack Chaula, mwenye umri wa miaka 24, kifungo cha miaka miwili jela au kulipa faini ya Shilingi milioni tano za Tanzania (takribani Dola 2,000 za Marekani) kwa kusambaza taarifa potofu kinyume na kifungo cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya mwaka 2015. Polisi walisema Chaula alitumia “meneno makali” dhidi ya rais katika video aliyoirusha kwenye mtandao wake wa TikTok mnamo Juni 30, 2024 akijionesha akichoma moto picha ya Rais Hassan huku akimtolea matusi. Watu wema walimchangia kiasi hicho cha faini, na kumwezesha kutoka jela. Hata hivyo, mnamo Agosti 2, 2024, alisemekana kutekwa na watu wasiojulikana na hajaonekana tena tangu hapo. Katika barua ya Agosti 8, 2024 kwa vyombo vya habari, Kamanda wa Polisi Moa wa Mbeya, Benjamin Kuzaga, alikiri kuwepo kwa tukio hilo na kuahidi kufanya uchunguzi⁸⁶, lakini hakuna taarifa rasmi iliyokwisha kutolewa kwa umma.

Sheria ya Makosa ya Mtandaoni, 2015 (Sheria na. 14 ya 2015) inataja kuwa ni kosa la jinai kwa aina mbalimbali za kujieleza mtandaoni kupitia makosa mbayo hayana tafsiri bayana kama vile “taarifa potofu” na maudhui ambayo yanaweza “kusababisha hofu na taharuki.”⁸⁷ Vipengele hivi vinashindwa kukidhi matakwa ya kisheria, ulazima, na uwiano chini ya Ibara ya 19(3) ya ICCPR.

Mnamo Oktoba 2, 2024, Mamlaka ya Kudhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilisimamisha leseni za maudhui mtandaoni za chapa tatu za Mwananchi Communication Limited: The Citizen, Mwananchi Digital, and Mwanaspoti kwa siku 30 kufuatia kutolewa kwa kikaragushi na The Citizen kilichosambaa sana mtandaoni. Vyombo vingi vya habari pia vimekumbana na amri kutoka TCRA kuondoa maudhui yaliyochapishwa kwenye kurasa zao, ambayo yanahisiwa kupingana na msimamo au maelezo ya serikali, ikisababisha hofu kwa waandishi wa habari na wahariri.⁸⁸

Mnamo Juni 18, 2025 polisi jijini Dar es Salaam walimweka chini ya ulinzi Janeth Rithe, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake ya ACT Wazalendo, kwa siku nne baada ya kuitikia wito wa kufika polisi. Polisi walimwita Rithe kwa mahojiano kuhusu kauli aliyotoa Juni 18, 2025, kwenye mkutano wa hadhara, Manzese, Dar es Salaam, ambapo alielezea kushangazwa na madai ya Rais Hassan kwamba Tanzania ilikuwa ikifanya vizuri zaidi kiuchumi kuliko Marekani.⁸⁹

Mnamo Septemba 6, 2025, TCRA iliifungia JamiiForums kwa siku 90, jukwaa maarufu la mtandaoni, ikitaja kuchapishwa kwa maudhui ya kupotosha na ya kumkashifu Rais. Tuhuma za madai hayo zilisemekana kutokana na kuvunja Kanuni za Maudhui ya Mtandaoni za mwaka 2020 na marekebisho yake ya mwaka 2022 na 2025.⁹⁰ TCRA ilisema kwamba mnamo Septemba 4, 2025, JamiiForums ilichapisha maudhui ya kupotosha, kukashifu, na kuishushia hadhi Serikali na Rais kupitia tovuti yake na akaunti zake za mitandao wa kijamii.⁹¹ Kufungiwa kwa JamiiForums kulifuatia kesi ya jinai iliyokuwa ikiwakabili wamiliki wa chaneli ya YouTube iitwayo Wachokonozi, Jackson Kabalo na Joseph Mrindoko, ambao wanakibiliwa na mashtaka ya kuchapisha taarifa potofu kinyume na Kifungu cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya 2015, na kuchapisha maudhui mtandaoni bila ya leseni, kwa kukiuka Kifungu cha 116(3)(b) cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta.⁹²

Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Sura ya 306) na Kanuni zake kuhusu Maudhui Mtandaoni zinaweka takwa la usajili na kupata leseni kwa watengeneza maudhui wote wa mtandaoni, jambo linaloweza vikwazo vya kujieleza ambavyo haviendani na viwango vya kimataifa.⁹³ Vipengele vya

⁸⁶ Media Wire Express, Polisi Mbeya Kuchunguza Kupotea kwa Aliyechoma Picha, Agosti 9, 2024, mediawireexpress.co.tz/mbeya-police-probe-missing-accused-photo-burner/.

⁸⁷ Sheria ya Makosa ya Mtandaoni, 2015, Sheria ya 14 ya 2015, <https://tanzlii.org/akn/tz/act/2015/14/eng@2015-05-22>

⁸⁸ The Chanzo, “The Chanzo Yaondoa Maudhui ya Askofu Gwajima Kufuatia Wito wa TCRA,” Mei 27, 2025,

⁸⁹ Mwanahalisi Online, “ACT Wazalendo hawajui hatma ya Janeth Rithe,” Juni 21, 2025, mwanahalisonline.com/2025/06/21/act-wazalendo-hawajui-hatma-ya-janeth-rithe/

⁹⁰ Mahojiano kwa njia ya simu kati ya Amnesty International na Maxence Melo, Mkurugenzi Mtendaji wa Jamii Forums, Septemba 2025.

⁹¹ TCRA, taarifa kwenye Instagram, Septemba 25, 2025 (kwenye faili la Amnesty International).

⁹² The Chanzo, “Kesi ya Jinai Inayowakabili ‘Wachokonozi’ Yaahirishwa,” Agosti 14, 2025, thechanzo.com/2025/08/14/criminal-case-against-youtubers-wachokonozi-postponed/

⁹³ Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306, <https://tanzlii.org/akn/tz/act/2010/3/eng@2010-05-07>

kanuni hizo vinavyofanya mambo mengi kuwa kosa la jinai kutokana na maudhui ya kutengenezwa na watumiaji yanaunda hali ya kuwepo udhibiti mkubwa wa kinachochapishwa.

Wananchi wa kawaida pia wamelengwa chini ya kisingizio cha kupambana na upotoshaji wa taarifa. Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari (Sura ya 229) inatoa mamlaka kwa kuwepo kwa chombo cha kutoa leseni kwa maandishi wa habari na inatoa madaraka makubwa kwa Waziri mwenye dhamana kupiga marufuku maudhui yanayochukuliwa kuwa kinyume na "maslahi ya umma" au "usalama wa taifa."⁹⁴ Vipengele hivi vinakiuka kanuni ya uhalali wa kisheria chini ya Ibara ya 19(3) ya ICCPR kutokana na kukosa tafsiri thabiti na kuwa na viashiria vya madaraka makubwa kupita kiasi.

Mnamo Agosti 6, 2025, Waziri wa Mambo ya Ndani Innocent Bashungwa aliwaamuru polisi kufanya "doria mtandaoni,"⁹⁵ akidai hatua hiyo ingewafuatilia watu wanaodaiwa kutumia majukwaa ya kidigitali kuvuruga amani na usalama nchini Tanzania wakati huo huo kupambana na uhalifu wa mtandaoni.

Serikali imeongeza juhudi za kudhibiti huduma ya mitandao ya kijamii kuelekea uchaguzi mkuu. Mamlaka tayari zimekwisha finya upatikanaji wa mtandao wa X, ambao ni jukwaa linalopendwa na Watanzania kwa habari ambazo hazijafanyiwa mchujo na mijadala ya kisiasa. Watumiaji wa majukwaa mengine ya mtandaoni kama vile Telegram na Clubhouse nao pia wametoa taarifa ya kupata ugumu wa kuifikia mitandao hiyo, wengi wakisema lazima watumie VPN ili kuweza kushiriki katika mijadala.

"Hadi Machi 31, 2025, TCRA ilikuwa imebaini na kufungia jumla ya tovuti, kurasa za mitandao ya kijamii, majukwaa na blogu 80,171 ambazo zilikuwa zikichapisha maudhui yaliyochukuliwa kuwa kinyume cha maadili na yenye kudhuru afya ya akili ya watoto."⁹⁶

Mnamo Mei 5, 2025, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo aliliambia bunge kuwa TCRA ilikuwa imebaini na kufungia majukwaa 80,171 kwa "kuchapisha maudhui yaliyo kinyume cha maadili ambayo yana hatari kwa afya ya akili ya watoto."⁹⁷ Kulingana na NetBlocks, shirika linalofuatilia matumizi ya mitandao duniani, likijikita zaidi katika kuangalia uwiano wa haki za kidigitali, usalama wa kimtandao na udhibiti wa intaneti, mnamo Mei 20, 2025, vipimo vya matumizi mbashara vilionesha kwamba mtandao wa X ulikuwa haupatikani kwa watoaji wakubwa wa huduma za mtandao nchini #Tanzania. Tukio hilo lilifuatia machapisho ya akaunti za polisi katika X zilizodukuliwa yakidai kuwa Rais Hassan alikuwa amekufa⁹⁸. Hadi wakati wa kuchapisha taarifa hii, watumiaji waliweza tu kuipata X kupitia VPN.⁹⁹

Ibara ya 9 ya Mkataba wa Afrika inawahakikishia watu binafsi haki ya kupata habari pamoja na haki ya kujieleza na kusambaza habari. Mnamo Novemba 2019, Tume ya Afrika ilipitisha Azimio la Kanuni za Uhuru wa Kujieleza na Kupata Habari barani Afrika lililochukua nafasi ya Azimio ambalo Tume ya Afrika ilikuwa imelipitisha mwaka 2002. Azimio la 2019 linaimarisha mwendelezo kuhusu uhuru wa kujieleza na kupata habari kwa kuongozwa na viwango vinavyotokana na mikataba ya haki za binadamu ya Afrika na Kimataifa na vyombo vya kisheria vya Afrika.¹⁰⁰

Ushambuliwaji wa uhuru wa kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari unakiuka Ibara ya 19 ya ICCPR na UDHR ambayo inahakikisha uhuru wa kujieleza, pamoja na "uhuru wa kutafuta, kupokea na kuelezea habari na mawazo ya kila aina."¹⁰¹

⁹⁴ Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, Sura ya 229, <https://tanzlii.org/akn/tz/act/2016/12/eng@2016-11-18>

⁹⁵ Wizara ya Mambo ya Ndani, Bashungwa Amuagiza IGP kudhibiti wahalifu wanaotumia mitandao kuvuruga amani, Agosti 11, 2025, moha.go.tz/index.php/News/QK9b68neEv

⁹⁶ The Chanzo, TCRA Yafungia Zaidi ya Mitandao ya Kijamii 80,000 Yenye Maudhui Hatarishi kwa Watoto, Mei 5, 2025, www.youtube.com/watch?v=QUgOCYJrAqU

⁹⁷ The Chanzo, TCRA Yafungia Zaidi ya Mitandao ya Kijamii 80,000 Yenye Maudhui Hatarishi kwa Watoto, Mei 5, 2025, www.youtube.com/watch?v=QUgOCYJrAqU

⁹⁸ NetBlocks, Mei 20, 2025, mastodon.social/@netblocks/114541588493655020

⁹⁹ Mahojiano ya ana kwa ana kati ya Amnesty International na Watanzania wanne, Septemba 30, 2025.

¹⁰⁰ Tume ya Afrika, Azimio la kanuni kuhusu Uhuru wa Kujieleza 2019.

¹⁰¹ Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, "Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa," Ibara ya 19, www.ohchr.org/en/instruments-mechanisms/instruments/international-covenant-civil-and-political-rights

11. UMINYWAJI WA UHURU WA KUTEMBEA

Viongozi wa upinzani na wanaharakati wamekabiliwa na uminywaji mkubwa wa uhuru wao wa kutembea ambao umewazuia kabisa kufanya shughuli zao za kawaida za kisiasa.

Mnamo Januari 29, 2024, Mdude Nyagali alitoa taarifa kwamba mamlaka husika katika mpaka wa Tanzania na Kenya, Namanga zilimzuia kuondoka nchini kwenda Kenya baada ya kueleza kwamba ilimbidi apate kibali maalum kutoka vyombo vya sheria kabla ya kuondoka Tanzania.¹⁰²

Mnamo Mei 13, 2025, naibu katibu mkuu wa Chadema Amani Golugwa alitiwa mbaroni kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere alipokuwa akijiandaa kuelekea Brussels kupitia Shirika la Ndege la Uturuki kuhudhuria Mkutano wa Umoja wa Kidemokrasia wa Kimataifa.¹⁰³ Polisi walidai kwamba walikuwa wakitenda kutokana na taarifa za kiintelijensia kwamba Golugwa alikuwa "amejenga mazoea ya kutoka na kuingia nchini bila ya kufuata taratibu zilizowekwa."¹⁰⁴ Kulingana na Golugwa, polisi walidai kwamba amekuwa akituma habari nje ya nchi kwenda, miongoni mwa taasisi nyingine nyingi, kwa bunge la Ulaya. Walidai zaidi kwamba Golugwa amekuwa akibadilishana taarifa na wageni inayodhalilisha nchi, jambo lililosababisha Bunge la Ulaya kuiweka nchi baadhi ya vikwazo.¹⁰⁵

"Walinihoji kuhusu madai ya kupeleka taarifa nje ya nchi, hususani kwa watu binafsi wa Bunge la Ulaya. Walidai kwamba taarifa niliyoituma ilikuwa ya kudhalilisha nchi na inawezekana ilichangia kwa Bunge la Ulaya kuiweka vikwazo Tanzania."¹⁰⁶

Mnamo Juni 6, 2025, afisa mwandamizi wa Chadema Godbless Lema alizuiwa katika mpaka wa Namanga na maafisa wa uhamiaji na kuwekwa chini ya ulinzi kwa takribani saa nne wakati akielekea Nairobi, Kenya. Kulingana na maelezo aliyoyotoa kwa Amnesty International, alikuwa akielekea Nairobi kufanyiwa uchunguzi wa afya yake.¹⁰⁷ Alinyang'anywa pasipoti yake, na alishikiliwa kwa saa kadhaa kabla ya kuachiwa na kuamriwa kwenda Makao Makuu ya Uhamiaji Dodoma kwa maelezo zaidi. Idara ya Uhamiaji ilieleza hatua hiyo kuwa ni ya "kawaida," ambayo kwa kawaida huchukuliwa pale inapokuwa imepewa taarifa inayotaka mhusika kuhojiwa.¹⁰⁸

Mnamo Julai 12, 2025, maafisa waandamizi wawili wa Chadema, Brenda Rupia na Leonard Joseph Magere, walizuiwa kwenda nchi jirani ya Kenya kwenye mpaka wa Namanga baada ya kukamatwa na polisi. Polisi walithibitisha kumtia mbaroni Rupia, wakidai ilihusiana na uchunguzi kwa vile alidaiwa kuchapisha taarifa potofu kwenye mitandao ya kijamii.¹⁰⁹

Sheria ya Uhamiaji ya Tanzania, 1995 na kanuni husika zinatoa madaraka makubwa kwa maafisa wa uhamiaji kuyatumia wapendavyo na hayana uthabiti unaotakiwa chini ya sheria ya kimataifa kwa kuminya haki za msingi. Utaratibu uliopo kimaandishi wa kuhitajika "kibali maalum kutoka vyombo vya sheria" kwa wanachama wa upinzani kusafiri, kama alivyoamriwa Nyagali, hauna msingi ulio dhahiri wa kisheria na unakiuka kanuni ya uhalali wa kisheria.¹¹⁰

Uminywaji wa uhuru wa kutembea unakiuka Ibara ya 12 ya ICCPR, ambayo inasema kwamba "kila aliyepo kisheria katika ardhi ya mamlaka ya Dola, ndani ya ardhi hiyo, ana haki ya uhuru wa kutembea na uhuru wa kuamua ni wapi yawe makazi yake" na kwamba "kila mtu yupo huru

¹⁰² Mdude Nyagali, taarifa kwenye X, Januari 24, 2024, x.com/mdudenyagali/status/1751858280790417671?s=20

¹⁰³ The Chanzo, "Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Amani Golugwa Akamatwa Uwanja wa Ndege Akielekea Brussels katika Mkutano wa IDU," Mei 13, 2025, thechanzo.com/2025/05/13/chadema-deputy-secretary-amani-golugwa-arrested-at-airport-while-heading-to-idu-forum-in-brussels/

¹⁰⁴ Mahojiano kwa njia ya simu kati ya Amnesty International na Edgar Mwakabala, Mei 2025.

¹⁰⁵ Mahojiano kwa njia ya simu kati ya Amnesty International na Amani Golugwa, Septemba 2025.

¹⁰⁶ Mahojiano kwa njia ya simu kati ya Amnesty International na Amani Golugwa, Septemba 2025.

¹⁰⁷ Godbless Lema, taarifa kwenye X, Septemba 24, 2025, x.com/godbless_lem/status/1930979938804363683

¹⁰⁸ Idara ya Uhamiaji Tanzania, taarifa kwenye Instagram, Septemba 25, 2025.

¹⁰⁹ Polisi Tanzania, taarifa kupitia Gazeti Jamvi kwenye Facebook, Septemba 25, 2025, www.facebook.com/gazetijamvi/posts/baada-ya-chama-cha-demokrasia-na-maendeleo-chadema-kuandika-barua-ya-kudai-mwana/1306699944144645/

¹¹⁰ Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa, Ibara ya 12, www.ohchr.org/en/instruments-mechanisms/instruments/international-covenant-civil-and-political-rights

kuondoka katika nchi yoyote, ikiwemo ya kwake."¹¹¹ Uminywaji uliopo kimaandishi hauna msingi wa kisheria, ulazima na uwiano unaoitakiwa chini ya sheria ya kimataifa.

Ibara ya 12(1) ya Mkataba wa Afrika inasema kwamba kila mtu ana haki ya kutembea kwa uhuru na kuishi popote katika nchi yake, ili mradi tu anafuata sheria. Pia anayo haki ya kuondoka katika nchi yoyote, ikiwemo ya kwao, na kurejea nchini humo.¹¹² Mwaka 2019, Tume ya Afrika ilipitisha Maoni ya Jumla Na. 5 kuhusu Mkataba wa Afrika. Katika maoni ya jumla hayo, tume ilielezea kwa kina kuhusu haki ya uhuru wa kutembea na kuishi ndani ya mipaka ya nchi.¹¹³

11.1 KUDHARAU UHURU WA KUTEMBEA ULIOPO KIMKATABA

Ibara ya 104 ya Mkataba wa Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaangazia uzingatiaji wa nchi wanachama wa EAC kuchukua hatua za kurahisisha uhamaji wa watu, wafanyakazi, na huduma katika nchi wanachama. Inaunga mkono haki za raia kuishi, kufanya kazi na kuanzisha biashara popote ndani ya jumuiya.¹¹⁴

Mnamo Mei 18 na 19, 2025, mamlaka za uhamiaji za Tanzania ziliwakatalia kuingia nchini wanasheria na wanaharakati mashuhuri sita wa haki za binadamu wa Kenya—akiwemo Waziri wa Sheria wa zamani Martha Karua na Jaji Mkuu wa zamani Willy Mutunga—waliokuwa wamesafiri hadi Dar es Salaam kuhudhuria kesi ya uhaini ya kiongozi wa upinzani Tundu Lissu.

Kutowaruhusu kuingia nchini kulikiuka wajibu wa Tanzania chini ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Mkataba wa Soko la Pamoja (CMP), ambao unahakikisha uhuru wa kutembea kwa uhuru katika nchi wanachama. Kundi hilo lilijumuisha Martha Karua, Waziri wa Sheria wa zamani wa Kenya; Willy Mutunga, Jaji Mkuu wa zamani wa Kenya; Gloria Kimani, Mjumbe wa Halmashauri ya Chama cha Wanasheria wa Kenya na wanaharakati wa haki za binadamu Lynn Ngugi, Hussein Khalid na Hanifa Adan. Baada ya kuwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, watu hao walisemekana kuwekwa chini ya ulinzi bila ya maelezo, wakanyang'anywa pasipoti zao, na hatimaye wakarejeshwa Kenya.¹¹⁵ Ziara yao ilikuwa sehemu ya ujumbe wa waangalizi wa kesi hiyo wa kimataifa, lakini maafisa wa Tanzania walidai hawakuwa na vibali muhimu vya kufanya shughuli za kisheria au shughuli za utetezi nchini.¹¹⁶

12. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Gunduzi na mapendekezo katika ripoti hii yanaendana na yale yaliyotolewa katika ripoti ya Amnesty International ya mwaka 2020 "*Kutumia Sheria kama Silaha: Ukandamizaji wa Sheria kuelekea Uchaguzi Mkuu Tanzania*" ambazo zimegundua kwamba sheria zimetumika kuunda mfumo thabiti wa udhibiti wa kisiasa, zikiruhusu serikali ya Tanzania kudhibiti shughuli za upinzani, kukandamiza mawazo tofauti, na kudhibiti shughuli za kidigitali na kiuchumi. Huku zikioneshwa kama mabadiliko, matokeo ya jumla ya sheria mpya ni kupunguza uhuru wa kijamii kabla ya uchaguzi wa mwaka 2025.

Gunduzi katika taarifa hii zinaonesha mfumo ulioota mizizi sana wa ukandamizaji unaoongozwa na serikali ambao umeongezeka kwa wigo na ukubwa wake wakati Tanzania inapoelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Ukiukaji ulioainishwa—kuanzia utoweshwaji, mateso na uonevu mwingine hadi udhibiti wa maudhui ya mitandao na mashtaka ya jinai yenye msukumo wa kisiasa—si matukio

¹¹¹ Ofisi ya kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, "Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa," Ibara ya 12, <https://www.ohchr.org/en/instruments-mechanisms/instruments/international-covenant-civil-and-political-rights>

¹¹² Ibara ya 12(1) ya Mkataba wa Afrika.

¹¹³ Maoni ya Jumla ya Tume ya Afrika kuhusu Haki ya Uhuru wa Kutembea na Makazi chini ya Ibara ya 12(1) ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu.

¹¹⁴ Ibara ya 104, Mkataba wa Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Ibara ya 104, umesainiwa Novemba 30, 1999 na kuanza kutumika Julai 7, 2000.

¹¹⁵ Mahojiano kwa njia ya simu na ya ana kwa ana kati ya Amnesty International na Martha Karua, Willy Mutunga, Gloria Kimani, Lynn Ngugi, Hussein Khalid na Hanifa Adan, Mei 2025.

¹¹⁶ Waziri wa Katiba na Sheria wa Tanzania, Dkt. Damas Ndumbaro, alitetea kurejeshwa nchini kwao, akidai watu hao hawakuwa na vibali vya kufanya shughuli za kisheria au utetezi nchini Tanzania na hivyo walikuwa wamekiuka sheria za nchi.

yanayojitegemea bali ni sehemu ya mkakati wa makusudi wa kusambaratisha ushiriki wa kisiasa na kunyamazisha upinzani.

Muundo wa kisheria na kitaasisi Tanzania umesukwa upya ili kutumikia maslahi ya kisiasa, ukiwezesha serikali kuendesha shughuli zake bila ya uwajibikaji huku ikimomonyoa utawala wa sheria. Kwa mamlaka kukataa kutekeleza amri za mahakama, kulengwa kwa viongozi wa upinzani kupitia matumizi mabaya ya taratibu za kisheria, na kugeuza mifumo ya udhibiti kuwa silaha dhidi ya asasi za kiraia na vyombo vya habari kunaonesha muundo wa utawala ambao unazidi kuwa adui wa uwajibikaji na uwazi.

Taarifa hii inasisitiza kuwepo hitaji la haraka kwa wahusika wa ndani na wa kimataifa kutambua uzito wa hali halisi. Bila ya shinikizo la haraka na endelevu la kubadilisha mwenendo huo, ipo hatari ya uchaguzi wa mwaka 2025 kuwa zoezi la kiutaratibu ambalo halina uhalali, linalofanywa katika mazingira ambayo hofu, ukatili na kuenguliwa vimechukua nafasi ya ushindani wa wazi wa kisiasa.

MAPENDEKEZO

12.1 KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

- Thibitisha hadharani kwamba serikali itaheshimu, italinda, itaendeleza na kutekeleza haki za binadamu kabla, wakati na baada ya uchaguzi, haitavumilia ukiukaji wowote na uvunjaji wa haki za binadamu, na itahakikisha uchunguzi wa haraka, wa kina, wa wazi na fanisi wa madai yote ya ukikwaji na uvunjwaji wa haki za binadamu na kuwafikisha watuhumiwa mbele ya sheria.
- Laani hadharani vitisho vyote, udhalilishaji, unyanyasaji na ushambuliaji wa wanasiasa wa upinzani, viongozi wa kidini, watetezi wa haki za binadamu, wanaharakati, mashirika yasiyo ya kiserikali, vyombo vya habari, waandishi wa habari, na watumiaji wa mitandao ya kijamii na heshimu na kulinda haki ya uhuru wa kujieleza, kukusanyika kwa amani, na kujumika kwa watu wote.
- Tambua hadharani na linda umuhimu na uhalali wa kazi ya haki za binadamu inayofanywa na watetezi wa haki za binadamu, wanaharakati na mashirika ya asasi za kiraia, na hakikisha kwamba wanaweza kufanya kazi zao ka uhuru na kwa kujitegemea bila ya hofu ya kuadhibiwa.
- Hakikisha ufutwaji wa haraka na upitaji upya wa sheria na kanuni zote kandamizi zinazokiuka viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, ikiwemo Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, Sheria ya Makosa ya Mtandaoni, na Sheria ya Utulivu wa Umma na kuhakikisha sheria na kanuni zote kama hizo zinaendana na katiba ya Tanzania na wajibu na majukumu ya kimataifa ya haki za binadamu.
- Eleza hadharani kwamba serikali yako itachukua hatua kutekeleza Azimio la Umoja wa Mataifa la Watetezi wa Haki za Binadamu kuwa sheria ya nchi, na komesha udhalilishaji na unyanyasaji wa vyama vinavyotekeleza kazi yake kisheria ya kutetea haki za watu wengine.
- Toa majibu chanya, bila ya ucheleweshwaji zaidi kwa maombi yaliyotolewa na Taratibu Maalum za Umoja wa Mataifa (UN Special Procedures), ikiwemo Ripoti ya Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki ya uhuru wa kukusanyika kwa amani na kujumuika na Ripoti ya Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu kuendeleza na kulinda haki ya uhuru wa kutoa mawazo na kujieleza na hakikisha upatikanaji wake kamili usiokuwa na vizuizi.

12.2 KWA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI

- Fanya uchunguzi huru kuhusu matukio ya kutiwa mbaroni bila kufuata utaratibu wa sheria, utesaji na ukatili mwingine. Hakikisha uwajibikaji kwa watuhumiwa, toa msaada wa kitiba na kisaikolojia, na hakikisha uchukuaji wa hatua za kisheria za kulipwa fidia na kulindwa dhidi ya kulipiziwa kisasi katika siku za usoni kuhusiana na kesi za Abdul Nondo, Agather Atuhaire, Boniface Mwangi, Khadija Anwar Mohamed, Mwabili Mwangodi na Said Muhuzi Bakari.
- Komesha mara moja tabia ya utoweshwaji na toa maelezo ya hatma na walipo watu wote waliopotea, ikiwemo kufanya uchunguzi huru wa matukio yahusiyo utoweshwaji. Hakikisha uwajibikaji kwa watuhumiwa na thibitisha kutendewa haki kisheria na kulindwa dhidi ya kulipiziwa kisasi katika kesi za, Anthony Gabriel, Daniel Chonchorio, Deusdedith Soka, Dioniz Kipanya, Fakihi Ali Salim, Frank Mbise, Humphrey Polepole, Jacob Mlay, Mdude Nyagali, Shadrack Chaula, Sinda Mseti na Siza Mwita Keheta.
- Fanya uchunguzi huru kuhusu tukio la kuwekwa kizuizini na kushambuliwa kwa John Mnyika na hakikisha uwajibikaji kwa wahusika, toa msaada wa kitiba na kisaikolojia, na thibitisha uchukuaji wa hatua za kisheria za kulipwa fidia na kulindwa dhidi ya kulipiziwa kisasi siku za usoni.
- Fanya uchunguzi wa haraka, wa kina na usio wa upendeleo kuhusu madai yote ya ukiukaji wa haki za bindamu, ikiwemo shambulio la kimwili dhidi ya Charles Kitima na Edgar 'Sativa' Mwakabela, fikisha wahusika mbele ya sheria na thibitidha uchukuaji wa hatua za kisheria na kutendewa haki na kulindwa dhidi ya kulipiziwa kisasi katika siku za usoni.
- Fanya uchunguzi huru kuhusu matukio ya kutekwa, kuteswa, na mauaji bila ya kufuata utaratibu wa kisheria ya Ali Mohammed Kibao na thibitisha uchukuaji wa hatua za kisheria za kutendewa haki na kulindwa kwa familia yake dhidi ya kulipiziwa kisasi katika siku za usoni.
- Fanya uchunguzi huru kuhusu tukio linalohusiana na kukamatwa na kuzuiliwa kusafiri kwa Amani Golugwa, Brenda Rupia, Godbless Lema, Leonard Joseph Magere, Martha Karua, Willy Mutunga, Gloria Kimani, Lynn Ngugi, Hussein Khalid na Hanifa Adan ili kuhakikisha uwajibikaji kwa wahusika, na thibitisha uchukuaji wa hatua za kisheria kutendewa haki na kulindwa dhidi ya kulipiziwa kisasi katika siku za usoni.

12.3 KWA WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

- Hakikisha kuachiliwa huru mara moja na bila masharti kwa mtu yeyote aliyepo kizuizini kwa sababu tu ya kuelezea mawazo yake ya kisiasa na kidini au imani nyingine, ikiwemo Tundu Lissu na kufuta mashtaka yote dhidi yake, kwa vile yanaashiria kuchochewa na sababu za kisiasa.
- Rejesha upatikanaji wa mitandao ya kijamii na komesha uchujaji wa maudhui ya mtandaoni.
- Hakikisha kwamba vyombo vya habari vipo huru kufanya kazi kwa uhuru, na kwamba waandishi wa habari na wafanyakazi wengine katika vyombo vya habari wanaweza kufurhika haki zao za kibinadamu ikiwemo haki ya uhuru wa kujieleza na kupata habari na kufanya kazi zao bila woga wowote wa kuchukuliwa hatua kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

12.4 KWA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA

- Anzisha mara moja mfumo huru wa kuchunguza kwa haraka, kwa kina, kwa uwazi na kwa ufanisi madai ya kutumia nguvu kupita kiasi, kukamatwa kinyume cha utaratibu wa kisheria, na ukiukaji mwingine unaofanywa na polisi.

- Hakikisha mamlaka zinaheshimu, zinalinda, zinaendeleza na kutekeleza kikamilifu na bayana haki za binadamu za kila mmoja ikiwemo haki ya uhuru wa kujieleza, kujumuika na kukusanyika kwa amani.
- Fanya uchunguzi wa haraka, wa haki, kina, wa wazi na fanisi kuhusu madai yote ya vitisho na ukatili wa kimwili wanaofanyiwa viongozi wa upinzani na wafikishe watuhumiwa mbele ya sheria kwa mashtaka yanayozingatia haki.

12.5 KWA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

- Tekeleza kikamilifu amri za mahakama bila ya ucheleweshaji au upendeleo wa tafsiri, ikiwemo hukumu iliyomrejesha Luhaga Mpina kama mgombea urais kupitia chama cha ACT Wazalendo, ikitengua uamuzi wa kuenguliwa kwake na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC).
- Zingatia kujitegemea kwako kama ilivyoainishwa katika Katiba chini ya Ibara ya 74(11) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayosema kwamba Tume haitapokea maelekezo au kudhibitiwa na mtu yeyote au mamlaka. Hiyo inajumuisha kujiepusha na kutenda kazi kutokana na maelekezo ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali au mamlaka yoyote ya pembeni.
- Hakikisha kwamba vyama vyote vya siasa na wagombea wote wanaweza kufanya kampeni kwa uhuru bila ya kunyanyaswa, kutishwa, au kufanyiwa vurugu.
- Fanya uchunguzi huru, wa kina, wa wazi na fanisi kuhusu madai ya kuwepo matendo ya kinyume cha sheria yanayosababisha ukiukwaji wa haki za binadamu unaohusiana na uchaguzi na mwajibishe mtu yeyote anayehisiwa kuhusika.
- Ruhusu waangalizi huru kufanya kazi yao kwa uhuru ikiwemo kufuatilia mwenendo wa uchaguzi na mazingira ya haki za binadamu yanayohusiana na uchaguzi.

12.6 KWA VYAMA VYOTE VYA SIASA NA WAGOMBEA WOTE

- Kubali hadharani kuendelea kuheshimu haki za binadamu za kila mmoja kabla, wakati na baada ya uchaguzi, pamoja na haki ya uhuru wa kujieleza, kujumuika na kukusanyika kwa amani na bila hofu ya kuchukuliwa hatua za kisheria.

12.7 KWA WAANGALIZI WA UCHAGUZI

- Ongezea vipengele vya haki za binadamu katika uangalizi wenu wa uchaguzi na weka taarifa yenu hadharani, ikiwemo kushindwa kwa mamlaka kusahihisha makosa haraka na kwa uthabiti kulingana na viwango vya kimataifa na vya kikanda vya haki za binadamu.
- Jumuisha uhusishaji wa masuala ya haki za binadamu katika maeneo ambapo kuna malalamiko makubwa au ambapo kuna historia ya vurugu za uchaguzi.
- Angalia kwa makini athari za mazingira ya kiusalama kuhusiana na haki za binadamu kwa kuweka mkazo mahsusi kwa matendo yanayofanywa na vikosi vya usalama kutatua matatizo yoyote yanayoweza kujitokeza wakati wa kipindi cha uchaguzi, kusimamia maandamano ya kisiasa na mikutano kwa usalama na kuzuia kitendo chochote katika mchakato wa uchaguzi ambacho kinaweza kusababisha au kuchangia katika ukiukwaji au uvunjaji wa haki za binadamu.

12.8 KWA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

- Iwajibishe Tanzania kwa ukiukaji wa haki kinyume na kanuni za Mkataba wa EAC kuhusu demokrasia, utawala wa sheria, haki za binadamu kuhusiana na matukio ya kutekwa na kuondolewa nchini kwa nguvu ya Agather Atuhaire, Boniface Mwangi na Mwabili Mwangodi.
- Saidia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza wajibu wake wa utawala wa sheria kadri unavyoshahibiana na haki za binadamu chini ya Ibara ya 6(d) ya Mkataba wa EAC na kanuni husika zinazokubalika.
- Weka shinikizo kwa mamlaka kuheshimu, kulinda, kuendeleza na kutoa haki za binadamu za kila mtu ikiwemo haki ya uhuru wa kutembea, kujieleza, kujumuika na kukusanyika kwa amani.
- Zungumzia wasi wasi na mapendekezo ya Amnesty International yaliyoelezwa kwa kina hapo juu katika mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na himiza utekelezaji wake mara moja.
- Zungumzia kupitia taratibu bayana na sahihi ukiukwaji na uvunjaji wowote wa haki za binadamu ulioshuhudiwa, au tuhuma za ukiukwaji na uvunjaji wa haki za binadamu zilizopokelewa, ikiwemo namamlaka husika, kwa mfano Jeshi la Polisi la Tanzania na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na fanya marejeo ya hali halisi kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

12.9 KWA JUMUIYA YA MAENDELEO KUSINI MWA AFRIKA

- Saidia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanikisha utawala wa sheria na ahadi za utawala kadri zinazohusiana na haki za binadamu chini ya Ibara ya 4(c) ya Mkataba wa SADC.
- Shinikiza mamlaka kuheshimu, kulinda, kuendeleza na kutekeleza haki za binadamu za kila mmoja ikiwemo na haki ya uhuru wa kujieleza, kujumuika na kukusanyika kwa amani.
- Zungumzia hoja na mapendekezo ya Amnesty International yaliyoelezwa hapo juu katika shughuli zenu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na toa wito kutekelezwa kwake mara moja.
- Zungumzia, kupitia njia za wazi na sahihi, ukiukwaji na uvunjaji wowote wa haki za binadamu ulioshuhudiwa, au tuhuma za ukiukwaji na uvunjaji wa haki za binadamu zilizopokelewa, pamoja na mamamlaka husika, kwa mfano, Jeshi la Polisi la Tanzania na Tume Huru ya Uchaguzi ya Taifa, na fanya tathmini ya hali ilivyo kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

12.10 KWA UMOJA WA AFRIKA

12.10.1 MWENYEKITI WA TUME YA UMOJA WA AFRIKA

- Laani hadharani ongezeko la ukandamizaji na ukiukwaji na uvunjaji wa haki za binadamu nchini Tanzania, pamoja na vitisho, udhalilishaji, unyanyasaji na mashambulizi dhidi ya wanasiasa wa upinzani, viongozi wa dini, watetezi wa haki za binadamu, wanaharakati, mashirika yasiyo ya kiserikali, vyombo vya habari, waandishi wa habari na watumiaji wa mitandao.
- Toa wito kwa mamlaka za Tanzania kuheshimu, kulinda, kuendeleza na kutimiza haki za binadamu za kila mtu ikiwemo haki ya uhuru wa kujieleza, kujumuika na kukusanyika kwa amani, kulingana na Ibara ya 3(h) ya Sheria ya Uanzishwaji wa Umoja wa Afrika (AU).

- Hakikisha kwamba ikiwa au wakati Ujumbe wa Waangalizi wa Uchaguzi wa Umoja wa Afrika (AUEOM) unapotumwa kuangalia uchaguzi, unaweka katika maandishi ukiukaji na uvunjaji wa haki za binadamu uliofanyika kabla, wakati na baada ya uchaguzi.
- Zungumzia hoja na mapendekezo ya Amnesty International yaliyoelezewa hapo juu katika shughuli zenu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na toa wito kutekelezwa kwake mara moja.

12.10.2 TUME YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU

- Laani hadharani ongezeko la ukandamizaji na ukiukwaji na uvunjaji wa haki za binadamu nchini Tanzania, pamoja na vitisho, udhalilishaji, unyanyasaji na mashambulizi dhidi ya wanasiasa wa upinzani, viongozi wa dini, watetezi wa haki za binadamu, wanaharakati, mashirika yasiyo ya kiserikali, vyombo vya habari, waandishi wa habari na watumiaji wa mitandao.
- Toa wito kwa mamlaka kuheshimu, kulinda, kuendeleza na kutimiza haki za binadamu za kila mtu ikiwemo haki ya uhuru wa kujieleza, kujumuika na kukusanyika kwa amani, kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu.
- Fuatilia utekelezaji na uzingatiaji wa Tanzania wa Azimio Na. 640 (LXXXIV) la Tume la Julai 30, 2025 ambalo Tume ilizitaka mamlaka za Tanzania, miongoni mwa hatua nyingine nyingi, “kuhakikisha uhuru wa kujieleza na upatikanaji wa habari wakati wa kipindi cha uchaguzi” na kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza “kutumia haki yao ya kupiga kura katika mazingira yasiyokuwa na udhalilishaji, vurugu, au vikwavo vingine vyovyote.”
- Toa wito kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza kikamilifu Mwongozo wa Tume wa mwaka 2017 kuhusu Upatikanaji wa Habari na Uchaguzi barani Afrika.

12.11 KWA JUMUIYA YA KIMATAIFA

- Laani hadharani ongezeko la ukandamizaji na ukiukwaji na uvunjaji wa haki za binadamu nchini Tanzania ikiwemo vitisho, udhalilishaji, unyanyasaji na mashambulizi dhidi wanasiasa wa upinzani, viongozi wa dini, watetezi wa haki za binadamu, wanaharakati, mashirika yasiyo ya kiserikali, vyombo vya habari, waandishi wa habari, na watuamiaji wa mitandao.
- Toa wito kwa mamlaka kuheshimu, kulinda, kuendeleza na kutimiza haki za binadamu za kila mtu ikiwemo haki ya uhuru wa kujieleza, kujumuika na kukusanyika kwa amani.
- Toa wito kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza kikamilifu Maoni ya Jumla Na. 25 ya Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa kuhusu haki ya kushiriki katika shughuli za umma, haki ya kupiga kura na haki ya ufikio usawa wa huduma za umma.

Amnesty International ni shirika la watu milioni 10 ambalo huhamasisha ubinadamu wa kila mmoja wetu na kuendesha kampeni ya kuleta mabadiliko ili sisi sote tuweze kufurahia haki zetu za binadamu. Dira yetu ni kuwa na dunia ambayo wenye madaraka wanatimiza ahadi zao, wanaheshimu sheria za kimataifa na kuwajibishwa. Hatufungamani na serikali, itikadi ya kisiasa, maslahi ya kiuchumi, au dini yoyote na kwa sehemu kubwa tunafadhiliwa na wanachama wetu na michango ya watu binafsi. Tunaamini kwamba kwa kufanya kazi kwa mshikamano na kuwapenda watu kila mahali, tunaweza kubadilisha jamii zetu kuwa bora zaidi.

Mawasiliano


info@amnesty.org


facebook.com/
AmnestyGlobal


@Amnesty


amnesty.org



Amnesty International
Peter Benenson House
1 Easton Street
London WC1X 0DW,
Uingereza

Isipokuwa kama imebainishwa vinginevyo, maudhui yaliyo kwenye taarifa hii yamesajiliwa chini ya leseni ya Creative Commons (uhusishaji, si ya kibiashara, hakuna vinyambuo, ya kimataifa 4.0).

<https://creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/4.0/legalcode>

Pale ambapo taarifa inahusishwa na mmiliki mwingine wa hakimiliki tofauti na Amnesty International taarifa hii haitakuwa chini ya leseni ya Creative Commons.

Kwa maelezo zaidi, tembelea [ukurasa wa idhini](#) kwenye tovuti ya Amnesty International.

Fahirisi: 56/0376/2025

Imechapishwa: Oktoba 2025

Lugha halisi: Kiingereza

© Amnesty International 2025